ewura CCC
Consumer Consultative Council

# Mtumiaji

*Jarida la habari zenye kuwajengea uelewa watumiaji wa huduma za Nishati na Maji*

ISSN 2738-9014

Toleo Na. 12 • **Julai - Desemba,** 2025

HALIUZWI



## Rais Samia aongoza Wiki ya Maji 2025

## Nishati Safi ya Kupikia ndiyo mpango mzima



# Kutoka Ofisi ya Katibu Mtendaji

Mpendwa Msomaji,

Ni furaha kubwa kukukaribisha katika Toleo la 12 la Jarida la Mtumiaji – jarida lako lenye taarifa muhimu na makala makini zinazolenga kukuongezea uelewa kuhusu huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa hapa nchini, kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2025.

Katika toleo hili, utapata kufahamu kwa undani kazi na mafanikio ya Baraza katika kuelimisha watumiaji wa huduma, kushiriki katika utatuzi wa malalamiko yao, na kuhamasisha mabadiliko chanya kuelekea matumizi ya nishati safi ya kupikia. Vilevile, tunakuletea simulizi halisi kutoka kwa baadhi ya wanufaika wa elimu ya mtumiaji, hadithi zinazogusa, kufundisha na kuhamasisha.

Tunakualika utenge muda wako kusoma, kutafakari, na kuwa sehemu ya safari ya kuijenga jamii yenye uelewa wa haki na wajibu wake, jamii inayoshiriki kikamilifu kuboresha huduma zinazotugusa sote.

Jarida la Mtumiaji ni zaidi ya machapisho, ni jukwaa la kujifunza, kutafakari na kushiriki mawazo. Kupitia kurasa zake, tunakukaribisha kufahamu kwa kina dhamira ya Baraza, na nafasi yako kama mtumiaji katika kuimarisha mfumo wa huduma kwa ustawi wa jamii ya watanzania.

Karibu uambatane nasi katika safari hii ya maarifa. Tunakutakia usomaji mwema na wenye tija.

**Bi. Stella K. Lupimo**
**KATIBU MTENDAJI**



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea Tuzo ya **Kinara wa Maji Afrika** kutoka kwa Waziri wa maji Mhe. Jumaa Aweso kwa niaba ya Taasisi ya WaterAid UK ya nchini Uingereza wakati wa hafla ya Kilele cha Wiki ya Maji na Uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Maji 2002, Toleo la 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City jijini, Dar es Salaam.*

# Rais Samia aongoza Wiki ya Maji 2025

## • Dkt. Biteko aeleza umuhimu wa kufanyia kazi changamoto
## • EWURA CCC yatoa elimu

**Na Mwandishi Wetu, Dar es Salaam**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameongoza kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Maji Duniani kwa mwaka 2025 yaliyofanyika kitaifa jijini Dar es Salaam tarehe 22 Machi, ambapo alisisitiza umuhimu wa kuhifadhi mazingira kama msingi wa upatikanaji endelevu wa huduma za maji kwa sasa na kwa vizazi vijavyo.

"Masuala ya maji sasa yamekuwa ajenda muhimu za kisiasa duniani kote. Ni lazima tuanze kuyashughulikia sasa ili tuwe tayari kwa kesho," alisema Rais Samia katika hotuba yake, akieleza jinsi mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri upatikanaji wa maji na maisha ya jamii.

Awali, tarehe 19 Machi 2025, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, alifungua rasmi maadhimisho hayo katika Ukumbi wa Mlimani City na kuzindua Taarifa ya Utendaji ya Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Dkt. Biteko alisema, "Taarifa hii inaonesha kuwa wastani wa upatikaji wa maji kwa sasa mijini ni asimia 84 na vijijini ni asilimia 79.6 ikiwa ni hatua kubwa katika kuuganisha watu na huduma za maji,"

Dkt. Biteko alibainisha miongoni mwa changamoto katika taarifa hiyo ikiwa ni upotevu wa maji na akazitaka mamlaka za maji kudhibiti changamoto hiyo. "Ni jukumu la mamlaka husika kufanyia kazi changamoto hii ili kuhakikisha maji yanayozalishwa yanawafikia watumiaji kuzipunguzia mamlaka gharama za uendeshaji," alisema Dkt. Biteko, huku akiipongeza EWURA kwa kazi nzuri ya udhibiti inayofanya.

Katika maonesho yaliyoambatana na maadhimisho hayo, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) lilishiriki kikamilifu kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu haki na wajibu wao kama watumiaji wa huduma za maji, pamoja na umuhimu wa kutunza mazingira kwa ajili ya huduma endelevu.

Kupitia banda lake la maonesho, EWURA CCC liliwahudumia wananchi wapatao 87 waliotembelea na kupata maelezo kuhusu namna ya kuwasilisha malalamiko ya huduma za maji, matumizi sahihi ya huduma hizo, na jinsi ya kushiriki katika uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa faida ya wote.

Kaulimbiu ya kitaifa ya mwaka huu ilikuwa "Uhifadhi wa Mazingira kwa Usalama wa Huduma za Maji", iliyoendana na kaulimbiu ya kimataifa "Uhifadhi wa Mifumo ya Barafu", iliyoangazia hatari ya kuyeyuka kwa barafu duniani na madhara yake kwa mfumo wa maji.

Maadhimisho haya yaliambatana pia na mikutano muhimu ya sekta ya maji, ikiwa ni pamoja na Mkutano wa Mapitio ya Sekta ya Maji uliofanyika tarehe 17 Machi 2025, na uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Maji uliofanyika tarehe 18 na 19 Machi, ambapo EWURA CCC ilishiriki katika mijadala ya kitaalamu na wadau mbalimbali.

Ushiriki wa EWURA CCC katika wiki hiyo unaendelea kuonesha dhamira ya Baraza katika kuhakikisha watumiaji wanapewa elimu ya kutosha kuhusu haki zao, wajibu wao, na nafasi ya kila mmoja katika kuhakikisha huduma za maji ni bora, endelevu na salama kwa wote.

# Baraza lavutiwa hatua za SUWASA kukabili changamoto za maji Singida



*Msimamizi Mwandamizi, Mradi wa Maji wa Miji 28 Mhandisi Lazaro Msaru, akiwaeleza Wajumbe wa Baraza kuhusu maendeleo ya Mradi wa uchimbaji kisima kirefu cha maji katika eneo la Mwankoko nje kidogo mwa mji wa Singida.*

**Na Lugiko L. Lugiko, Singida**

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), limeipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Singida (SUWASA kwa juhudu inazochukua kuboresha huduma za majisafi kwa wananchi wanaohudumiwa na Mamlaka hiyo.

Pongezi hizo zimetolewa na Mwenyekiti wa EWURA CCC Mha. David Ngula wakati wa ziara ya kikazi iliyofanywa na Wajumbe wa Baraza kwa lengo la kujionea hali halisi ya utoaji wa huduma za maji kwa wananchi wa mji wa  Singida na vitongoji vyake, pamoja na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira inayosimamiwa na SUWASA.

“Tuna wajibu wa kufuatilia huduma zinazotolewa na Mamlaka kwa watumiaji ili kuongeza uelewa wa Wajumbe wa Baraza. Ziara kama hizi hutuwezesha kuona kwa macho hali halisi ya huduma, na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi husika,” alisema Mhandisi Ngula.

Alisisitiza kuwa ziara hiyo ni sehemu ya mikakati ya Baraza katika kuhakikisha kuwa sauti ya mtumiaji inasikika, na changamoto zinazowakabili wananchi katika sekta za nishati na maji zinawasilishwa kwa wakati na kwa njia ya kudumisha mahusiano imara miongoni mwa wadau.

“Kwa kufanya hivyo, Baraza linaendelea kuwa kiunganishi muhimu kati ya watumiaji na watoa huduma, na kuimarisha misingi ya uwajibikaji, ushirikishwaji, na uboreshaji wa huduma kwa maendeleo endelevu ya jamii,” aliongeza.

Akitoa taarifa kwa ujumbe wa Baraza, Mkurugenzi Mtendaji wa SUWASA, Ndugu Sebastian Warioba, alisema changamoto kubwa inayoikabili Mamlaka hiyo kwa sasa ni upungufu wa uzalishaji wa maji ukilinganisha na mahitaji halisi ya wakazi wa mji wa Singida.

“Kwa sasa, uwezo wa uzalishaji ni lita milioni 10.5 kwa siku, wakati mahitaji halisi ni lita milioni 23.3 kwa siku. Hii inaonyesha wazi pengo kubwa la huduma,” alisema Warioba.

Alieleza kuwa, kupungua kwa uzalishaji huo kumetokana na baadhi ya visima kupungua uwezo wake, akitolea mfano Kisima cha Irao ambacho  awali kilikuwa kinachangia kiasi kikubwa cha maji.

Hata hivyo, alibainisha kuwa, SUWASA imechukua hatua madhubuti kukabiliana na hali hiyo, kupitia utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Miji 28, unaojumuisha uchimbaji wa visima vipya 12 pamoja na kufufua visima vilivyokuwa havitumiki.

Aidha, Mkurugenzi huyo alieleza ujumbe wa Baraza kuwa, Mamlaka hiyo iko katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka, mradi unaolenga kuimarisha usafi wa mazingira na kulinda afya za wakazi wa mji wa Singida.

“Mradi huu wa mabwawa ni sehemu ya juhudi za Serikali kupitia SUWASA kuhakikisha mji unakuwa safi na wenye mazingira salama kwa wakazi wake,” aliongeza Warioba.

Warioba alileza kuwa, pamoja na hayo, SUWASA imeendelea kutoa huduma ya maji salama kwa kuhakikisha kuwa maji yote yanatibiwa kabla ya kufikishwa kwa wananchi, ili kuepusha milipuko ya magonjwa ya tumbo na kulinda maisha ya watumiaji.

# EWURA CCC yavunja rekodi

Na Lugiko L. Lugiko, Dodoma

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limeweka rekodi mpya ya utekelezaji wa majukumu yake katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025, likionesha mafanikio makubwa katika maeneo ya utoaji elimu kwa umma, uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia, na elimu kuhusu haki na wajibu wa mtumiaji.

Akifafanua mafanikio hayo kupitia taarifa za utendaji kwa katika kipindi tajwa, Katibu Mtendaji wa Baraza, Bi. Stella Lupimo, amesema kuwa, Baraza limefanikiwa kutekeleza programu 610 za uelimishaji na kufikia watumiaji 127,020 sawa na ongezeko la asilimia 41.1 ya lengo la kufikia watumiaji 90,000 lililokuwa limewekwa, huku likishiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za utatuzi wa takribani malalamiko 2,135 kwa kushirikiana na watoa huduma na Mdhibiti EWURA.

Akizungumzia mchango wa Baraza katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia bi Lupimo alisema, "Baraza limeshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia kwa kuendesha programu za uhamasishaji kwenye mikoa 21 ya Tanzania Bara, programu zilizojikita katika kutoa elimu kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya nishati isiyo salama, huku likihamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia."

> **"Tumejipanga si tu kama sauti ya mtumiaji, bali kama daraja kati ya wananchi na watoa huduma. Tunaamini kuwa ufanisi wa huduma katika sekta hizi muhimu hauwezi kufikiwa bila ushiriki wa watumiaji katika kutoa maoni, kuhoji...**

Aliongeza kuwa programu hizo, ziliambatana na usambazaji wa machapisho 12,912 yenye taarifa na elimu kwa watumiaji ili kuongeza wigo wa kujifunza zaidi.

Alisema kuwa, mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano wa karibu na wadau mbalimbali katika sekta za nishati na maji.

"Tumejipanga si tu kama sauti ya mtumiaji, bali kama daraja kati ya wananchi na watoa huduma. Tunaamini kuwa ufanisi wa huduma katika sekta hizi muhimu hauwezi kufikiwa bila ushiriki wa watumiaji katika kutoa maoni, kuhoji, na kuelewa haki na wajibu wao, pamoja na mwitikio chanya wa watoa huduma," alisisitiza Bi. Lupimo.

Katibu Mtendaji huyo aliongeza kuwa Baraza linaendelea kuzishirikisha Kamati zake kote Tanzania Bara ili kufanikisha malengo ya kufikia watumiaji wengi zaidi kwa elimu na hamasha ya matumizi endelevu ya huduma za nishati na maji.



*Meneja Uzalishaji Maji na Usambazaji Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida, ndugu Elisha Kivuyo, akitoa maelezo kwa Ujumbe wa Baraza ulipoitembelea Mamlaka hiyo hivi karibuni.*

# WCRD 2025: EWURA CCC yasisitiza huduma bora

**Na Mwandishi Wetu, Morogoro**

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma Zinazodhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) limeendelea kudhihirisha dhamira yake ya kulinda haki za watumiaji kwa kushiriki kwa mafanikio makubwa katika maadhimisho ya Siku ya Mtumiaji Duniani (World Consumer Rights Day) yaliyofanyika kitaifa mjini Morogoro tarehe 15 Machi 2025.

Katika maadhimisho hayo yaliyobeba kaulimbiu ya "Haki na Maisha Endelevu kwa Mtumiaji", EWURA CCC liliungana na wadau wengine wakuu kama Jukwaa la Watumiaji Tanzania (TCF), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA), kwa lengo la kuelimisha, kusikiliza na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.

Kilele cha maadhimisho hayo kilichofanyika kwa njia ya kongamano kiliwakutanisha wadau 79 kutoka taasisi za umma na mashirika yasiyo ya kiserikali, ambapo EWURA CCC iliwasilisha mada mahsusi iliyobeba ujumbe wa "Wajibu wa Wadau Sekta za Nishati na Maji katika Kuimarisha Haki za Mtumiaji kwa Maisha Endelevu," ikiwa ni sehemu ya mchango wake katika kukuza uelewa wa haki, wajibu na nafasi ya mtumiaji kwenye maendeleo endelevu.

Akizungumza wakati wa uwasilishaji wa mada hiyo, Katibu Mtendaji wa EWURA CCC, Bi. Stella Lupimo, alisema "Ni vigumu kuwa na huduma bora za nishati na maji ikiwa wadau wote katika sekta hizi hawatashiriki kikamilifu kubadili mwelekeo na kuzingatia matumizi salama na endelevu."

Aliongeza kuwa kila mdau wa sekta wa sekta za umeme, mafuta, gesi asilia na maji ana jukumu la kulinda haki za watumiaji kwa maendeleo endelevu ya jamii na taifa kwa ujumla.

Maadhimisho hayo yaliambatana pia na mijadala ya moja kwa moja iliyorushwa kupitia YouTube na X (zamani Twitter) za Mwananchi Digital, ambapo EWURA CCC ilihamasisha matumizi sahihi ya nishati, ulinzi wa mazingira, na uboreshaji wa huduma zinazodhibitiwa.

Katika kongamano hilo, baadhi ya washiriki walieleza changamoto mbalimbali zinazowakabili, ikiwa ni pamoja na ucheleweshwaji wa fidia kwa wakazi wa Mazimbu Darajani waliounguliwa vifaa kutokana na hitilafu ya umeme.

Akijibu hoja hiyo, Afisa Uhusiano wa Wateja kutoka TANESCO, Bw. Hussein Kachwamba, alisema, "Bado hatujapokea malalamiko yoyote kutoka kwa wakazi katika eneo hilo kuhusu changamoto hiyo," huku akisisitza kupatiwa maelezo zaidi kuhusu njia iliyotumika kuwasilisha malalamiko hayo ili aweze kufuatilia suala hilo.

Kwa upande wa sekta ya maji, baadhi ya wakazi walilalamikia uhaba wa maji kutokana na uharibifu wa miundombinu ya maji unaosababishwa na uchimbaji holela wa barabara.

Akitoa majibu kwa niaba ya MORUWASA, Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja, Bw. Lyangonyo Kiguhe, alisema, "Ucheleweshaji wa kurekebisha mabomba yanayovuja mara nyingi husababishwa na ukosefu wa uratibu mzuri na TARURA. Matengenezo ya Barabara mara nyingi hufanywa bila kushirikiana na MORUWASA ili kubaini miundombinu ya mabomba iliyo chini ya ardhi."

Aidha, Bw. Kiguhe alifafanua kuwa urejeshaji wa huduma baada ya mabomba kupasuka huhitaji gharama kubwa, hivyo kulazimu uwepo wa majadiliano kati ya MORUWASA na TARURA ili kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati.

Akijibu swali kuhusu mkakati wa Baraza wa kufikia wadau wengi zaidi ili kuwapa elimu, Afisa Mwandamizi Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC, Bi. Chipegwa Samwel, alisema, "Baraza limekuwa likitumia majukwaa ya redio, mitandao ya kijamii, shule na taasisi za elimu ya juu pamoja na machapisho kama Jarida lake la "Mtumiaji" ili kuwafikia wananchi wengi zaidi, na kwamba jitihada hizo zitaendelea kutumika siku zijazo."

Akihitimisha kilele cha maadhimisho hayo, Mwenyekiti wa Jukwaa la Watumiaji Tanzania na Katibu Mtendaji wa LATRA CCC, Bw. Daud G. Daud, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa taasisi katika kuimarisha haki za watumiaji, akisema "Haki za mtumiaji ni msingi wa maendeleo jumuishi. Tushirikiane kuzijenga na kuzilinda kwa pamoja."




*Katibu Mtendaji wa EWURA CCC Bi. Stella Lupimo (katikati) akifafanua jambo wakati wa mkutano na waandishi wa habari ulioandaliwa na Jukwaa la Watumiaji Tanzania (TCF) kuelekea kilele cha Siku ya Mtumiaji Duniani, 2025*







**BODI YA UHARIRI**
Bi. Stella K. Lupimo - Mwenyekiti na Mhariri Mkuu
Geofrey Sokesia - Mhariri Msanifu
Lugiko L. Lugiko - Mjumbe
Chipegwa Samwel - Mjumbe
Anadoris Komba – Mjumbe
Emmanuel Chagu Paul - Mjumbe

**Wachangiaji**
Amani Mbogo
Anadoris Komba
Brenda Magoma
Catherine Charles Ochido
Chipegwa Samwel
Emmanuel Paul
Geofrey Sokesia
Lugiko Lugiko
Magreth Temba
Mwasiti Athumani
Neema Nnko
Noela Ntiluvakule
Nuru Zuberi
Ramadhan Kakende
Said Ismail
Sakina Yusuf
Theresia Mande
Wadi Omari
Zamda Mabada

**Mawasiliano**
**Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji**
Jengo la PSSSF, Mtaa wa Kambarage, Barabara ya Jakaya Kikwete,
S.L.P. 772, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 026 296 0099
Simu: +255 746 482 008
Baruapepe: info@ewuraccc.go.tz
Tovuti: www.ewuraccc.go.tz
EwuraCCC

# Elimu ya Mtumiaji: Nguzo ya Mabadiliko Endelevu

Katika muktadha wa uboreshaji wa huduma za nishati na maji, elimu kwa mtumiaji inabaki kuwa msingi thabiti wa kujenga jamii yenye uelewa, inayowajibika, na inayochochea maendeleo endelevu. Uelewa wa haki na wajibu wa mtumiaji haupaswi kuchukuliwa kama jambo la hiari, bali kama hitaji la msingi linalohitaji kupewa kipaumbele katika sera, mipango na utekelezaji wa huduma za kijamii.

Ili elimu hiyo iwe na tija, kunahitajika mfumo madhubuti wa usimamizi, utekelezaji wenye mwelekeo wa pamoja, na ushirikiano wa karibu kati ya Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), watoa huduma, wadau wa maendeleo, na wananchi wenyewe.

Katika muktadha huu, EWURA CCC inajitokeza kama kiunganishi muhimu kati ya wananchi, watoa huduma, na Mamlaka ya Udhibiti. Baraza limekuwa likifanya zaidi ya kutoa wito kuhusu haki za watumiaji, limekuwa likiwafikia moja kwa moja, linasikiliza maoni yao, linawawezesha kwa elimu, na kuwahamasisha kuchukua hatua za kuboresha huduma za nishati na maji kwa njia endelevu.

Kupitia mikutano ya hadhara, vipindi vya redio na televisheni, machapisho ya elimu, na matumizi ya mitandao ya kijamii, Baraza limekuwa mstari wa mbele katika kuhimiza matumizi salama na endelevu ya huduma za nishati na maji. Juhudi hizi zimejikita pia kwenye kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ikiwemo gesi asilia, umeme, na majiko banifu ili kupunguza athari za kiafya na kimazingira.

Baraza linaamini kuwa maendeleo ya kweli hayawezi kutegemea uwepo wa miundombinu pekee. Badala yake, mafanikio ya huduma yanategemea mabadiliko ya fikra za jamii kuhusu matumizi sahihi na utunzaji wa miundombinu hiyo. Tabia kama uharibifu wa miundombinu, wizi wa mita na mafuta ya transfoma, au uchafuzi wa vyanzo vya maji, si tu kwamba zinadhoofisha huduma, bali pia zinahatarisha maisha na ustawi wa wananchi.

Ni wakati muafaka kwa wananchi kuacha visingizio na kuchukua hatua madhubuti. Tujiulize kama tunalinda au tunahujumu huduma zinazotutegemea sisi wenyewe. Kuchagua kutumia nishati safi ya kupikia, kuacha vitendo vya kuhujumu miundombinu, na kuwa walinzi wa rasilimali zetu ni wajibu wa kizalendo unaopaswa kuendelezwa kwa vitendo.

Ni wazi kuwa elimu ya mtumiaji ni silaha ya mabadiliko chanya. Kwa kuwekeza kwenye uelewa wa wananchi kuhusu haki na wajibu wao, tunaijenga jamii imara inayoweza kushiriki kikamilifu katika maboresho ya huduma na kusimamia uwajibikaji wa watoa huduma. Huu ni wakati wa kuchukua hatua. Tujifunze, tuelewe, tushirikiane, na tulinde huduma hizi kwa manufaa ya sasa na kwa vizazi vijavyo.

Uelimishaji

# Matumizi salama ya nishati na maji yaingia madarasani

Na Mwandishi Wetu, Iringa

Katika jitihada za kuwajengea uelewa wa kina vijana wa kitanzania kuhusu matumizi bora ya rasilimali za nishati na maji, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Iringa, hivi karibuni liliendesha kampeni maalum ya utoaji elimu kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Lugalo, iliyopo Kata ya Gangilonga, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.

Akizungumza wakati wa kutoa elimu hiyo, Afisa Huduma kwa Wateja kutoka EWURA CCC Iringa, Bi. Brenda Magoma alieleza kuwa, kundi la wanafunzi ni la muhimu kuelimishwa mapema ili wawe mabalozi wa mabadiliko katika familia na jamii zao.

"Elimu hii inalenga kuwajengea msingi wa uelewa kuhusu matumizi sahihi ya hudumaili wanafunzi waweze kuepuka matumizi mabaya ambayo husababisha gharama zisizo za lazima, na pia waweze kudai haki zao kwa njia halali wanapohisi huduma wanazopata hazikidhi viwango," alisema Bi. Magoma.

Aliongeza kuwa, katika uelimishaji huo wanafunzi walifundishwa namna ya kutumia umeme na gesi kwa usalama, ikiwa ni pamoja na kutotumia vifaa vya umeme vilivyoharibika, kuzima vifaa visipotumika, kuhakikisha vali za gesi zimefungwa vizuri baada ya matumizi, na kuepuka kuwasha moto karibu na mitungi ya gesi.

> **Tumewaelimisha wanafunzi kuhusu matumizi salama ya umeme na gesi, matumizi ya maji kwa uangalifu ili kuepuka upotevu, pamoja na utaratibu wa kuwasilisha na kushughulikia malalamiko pale wanapokutana na changamoto katika huduma husika**

Bi Magoma alisisitiza pia umuhimu wa kuripoti kuhusu miundombinu ya maji inayovuja, ili kuzuia upotevu wa maji na gharama zisizo za lazima kwa familia.

"Tumewaelimisha wanafunzi kuhusu matumizi salama ya umeme na gesi, matumizi ya maji kwa uangalifu ili kuepuka upotevu, pamoja na utaratibu wa kuwasilisha na kushughulikia malalamiko pale wanapokutana na changamoto katika huduma husika," aliongeza Bi. Magoma.

Kwa upande wake, Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Iringa, Bw. Charles Lwabulala, alisisitiza kuwa, matumizi salama ya nishati nyumbani ni suala la msingi linalohitaji uelewa wa kiusalama kwa kila mtumiaji, wakiwemo wanafunzi.

Naye Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule hiyo, Bi. Rahel Mwinuka, aliishukuru EWURA CCC kwa kuchagua shule yao kufikishiwa elimu hiyo muhimu. "Tunathamini elimu tuliyopata leo kwani itasaidia walimu na wanafunzi kubadilisha mwenendo wa matumizi ya huduma hizi, si shuleni tu, bali hadi majumbani," alisema Bi. Mwinuka.

Kupitia kampeni hiyo, jumla ya wanfaunzi 670 na walimu 40 walifikiwa.

EWURA CCC inazidi kuthibitisha dhamira yake ya kuifikia jamii kupitia makundi mbalimbali ya watumiaji, hasa kupitia taasisi za elimu na makundi ya vijana, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake ya kisheria ya kusambaza taarifa muhimu zenye maslahi kwa watumiaji wa huduma za nishati na maji.



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Iringa Bw. Charles Lwabulala akitoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Lugalo iliyopo Manispaa ya Iringa.*



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Kagera ndugu Lenas Katabazi akielimisha wakazi wa Mtaa wa Mtoni kuhusu haki na wajibu wa watumiaji wa huduma za nishati na maji.*

# Viongozi Serikali za Mitaa kuiunga mkono EWURA CCC

**Na Anadorice Komba, Kagera**

Wenyeviti wa Serikali za mitaa Manispaa ya Bukoba, wameahidi kuendeleza ushirikiano na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), kwa kushirikiana katika mikutano yao ya mitaa, ili kuhakikisha elimu ya haki na wajibu wa watumiaji wa huduma za nishati na maji inasambaa kwa jamii wanazoziongoza.

Ahadi hiyo ilitolewa na Bw. Audax Rwechungura, Mwenyekiti wa Mtaa wa Bugambakamo, wakati wa mikutano ya mtaa ambayo EWURA CCC ilialikwa kushiriki hivi karibuni.

Ndugu Rwechungura alisema kuwa, EWURA CCC ni mdau muhimu ambaye kwa miaka mingi wamekuwa na ushirikiano wa karibu katika kuelimisha jamii kuhusu huduma za nishati na maji kupitia mikutano mbalimbali inayopangwa na serikali za mitaa.

"Kila baada ya miezi mitatu katika mtaa wetu huwa tunaita mkutano wa wananchi ambapo tunahakikisha wataalamu mbalimbali wanahudhuria kutoa elimu kwa wananchi," alisema Rwechungura.

Aliongeza kuwa, kupitia ushirikiano na EWURA CCC, wananchi wamepata uelewa mzuri kuhusu haki, wajibu wa watumiaji wa huduma za nishati na maji, njia bora za kutumia huduma hizo, na utaratibu wa kuwasilisha malalamiko.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Bugambakamo, Bw. Juvian Fabian, alikiri kutambua na kuthamini mchango chanya wa Baraza kwa wakazi wa mtaa wake.

"Elimu inayotolewa na EWURA CCC imekuwa ni chachu ya mabadiliko kwani wananchi wetu sasa wanatambua haki na wajibu wao kama watumiaji wa huduma za nishati na maji. Tunashukuru kwa ushirikiano huu na tunaahidi kuendelea kuupa nguvu katika mikutano yetu ya mitaa," alisema Bw. Fabian.

Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoa wa Kagera, Bw. Eustadi Katunzi, aliwashukuru wenyeviti hao kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa Baraza mkoani humo.

"Tunawashukuru sana wenyeviti kwa ushirikiano mnaoendelea kuutoa kwa Baraza hapa Kagera. Ushirikiano wenu ni nguzo muhimu kwa mafanikio katika kuwatetea na kuwaelimisha watumiaji wa huduma za nishati na maji," alisema Bw. Katunzi na kuongeza kuwa kupitia mikutano hiyo Baraza limefikia watumiaji 1,143 na kuwaelimisha.





*Afisa Huduma kwa Wateja EWURA CCC Mkoa wa Ruvuma Bi. Magreth Temba, akitoa elimu kwa wakazi wa mtaa wa Chemchem kuhusu umuhimu wa kuwasilisha malalamiko yanayohusu huduma za nishati na maji kwa watoa huduma husika.*

# Huduma za EWURA CCC ni bure

**Na Magreth Temba, Ruvuma**

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Ruvuma (Ruvuma RCC), kupitia mikutano ya uhamasishaji kwa wananchi wa Kata ya Seedfarm, Mtaa wa Ruhila, imewahimiza wakazi hao kuitumia Ofisi ya Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) iliyopo mjini Songea, kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali zinazohusu huduma hizo, kwa kuwa huduma zinazotolewa na Baraza ni bure.

Akizungumza wakati wa mikutano hiyo ya utoaji elimu iliyoendeshwa kwa ngazi ya mabalozi wa nyumba kumi katika Kata hiyo, Bw. Cryson Ngelangela, Mjumbe wa RCC Ruvuma alisisitiza kuwa, Baraza lipo kwa ajili ya kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA, zikiwemo umeme, maji, mafuta ya petroli na gesi asilia.

"Huduma zetu zote, kuanzia utoaji elimu, upokeaji wa malalamiko hadi kufuatilia ufumbuzi wake, hutolewa bure. Lengo letu ni kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za nishati na maji, na anaelewa kuwa ana haki ya kutoa malalamiko na kupata msaada bila kutozwa chochote," alisema Bw. Ngelangela.

Aliongeza kuwa, wananchi wengi wamekuwa wakikumbwa na matatizo kama bili kubwa za maji, kukatika kwa umeme bila taarifa, au upatikanaji usioridhisha wa maji, lakini hawajui pa kupeleka malalamiko yao. Aliwahimiza kuwasilisha malalamiko yao mara moja kwa watoa huduma na kwamba EWURA CCC iko tayari kuwasaidia katika ufuatiliaji wa utatuzi wa malalamiko hayo.

Naye Bi. Amina Salum, Katibu wa Wazazi wa CCM na mkazi wa Ruhila, alieleza kufurahishwa kwake na elimu waliyoipata kutoka EWURA CCC. "Nimefurahi kusikia kwamba huduma mnazotoa ni bure kwani awali tulidhani tungetozwa fedha kupata msaada katika ofisi yenu ikiwemo kufuatilia malalamiko, lakini sasa mmetuondolea hofu hiyo," alisema Bi. Salum.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Ruhila Ndugu Charles Akim, alilipongeza Baraza kwa kushiriki kikamilifu katika mikutano yote ya balozi katika mtaa huo. Alisema elimu waliyoitoa imekuwa na manufaa makubwa kwa wananchi wake, si tu kuhusu haki zao, bali pia kuhusu matumizi salama ya nishati safi ya kupikia.

"Mkutano huu umetufumbua macho kuhusu haki zetu na wajibu wetu kama watumiaji, zikiwemo haki ya kupata huduma, pamoja na kufidiwa. Pia tumepata uelewa kuhusu matumizi salama ya gesi za kupikia majumbani kama vile kuhakikisha kuwa mipira ya gesi haivuji, jambo ambalo ni muhimu hasa katika usalama wetu," alisema Bw. Akim.

Kupitia mikutano hiyo ya uelimishaji, Baraza limewafikia zaidi ya wananchi 400 katika Mtaa wa Ruhila ambapo walipatiwa elimu kuhusu majukumu ya Baraza katika kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji, namna ya kuwasilisha malalamiko, na matumizi endelevu ya huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.



# EWURA CCC na 'TK Movement' wapaza sauti kwa vijana

**Na Mwandishi wetu, Tanga.**

Zaidi ya vijana 1,000 kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Tanga wamepatiwa elimu ya matumizi salama na endelevu ya nishati safi ya kupikia, kupitia kampeni maalum ya uhamasishaji iliyoendeshwa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), kwa kushirikiana na taasisi ya Taifa Letu, Kesho Yetu Movement (TK Movement) ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia (2024–2034).

Kampeni hiyo, iliyolenga kuchochea mabadiliko ya tabia na kuongeza matumizi ya nishati safi kama gesi, umeme na majiko banifu miongoni mwa vijana, ilifanyika mwezi Aprili 2025 katika Ukumbi wa Samia Complex, Tanga na kufunguliwa na Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Mheshimiwa Zephania Sumaye, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tanga.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Afisa Mwandamizi wa Huduma kwa Wateja kutoka EWURA CCC Tanga, Bi. Nuru Zuberi, alisema elimu hiyo inalenga kuwajengea vijana msingi wa uelewa utakaowawezesha kuchagua njia bora za kupikia ambazo hazihatarishi afya wala mazingira.

"Matumizi ya nishati isiyo salama kama kuni na mkaa yana athari kubwa kwa afya, hususan kwa wanawake na watoto wa kike, lakini pia huharibu mazingira na kuongeza gharama za maisha. Vijana ni kundi muhimu katika kusukuma mabadiliko ya kitaifa, hivyo elimu hii inalenga kuwapa maarifa ya kuchukua hatua sasa," alisema Bi. Nuru.

Aliongeza kuwa, EWURA CCC itaendelea kushirikiana na taasisi za vijana na mashirika ya kiraia kueneza ujumbe wa matumizi ya nishati safi, sambamba na kutoa elimu kuhusu haki na wajibu wa mtumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA.

Kwa upande wake, Mratibu wa TK Movement Mkoa wa Tanga, Bi. Swaumu Ramadhani Tukuku, alipongeza EWURA CCC kwa ushirikiano wake katika kuwawezesha vijana kuwa mabalozi wa mabadiliko katika familia na jamii zao.

"Elimu waliyoipata vijana leo si tu inawawezesha kufanya maamuzi sahihi ya kiafya na kimazingira, bali pia inawaweka kwenye nafasi ya kuhamasisha wengine katika mitaa wanayoishi," alisema Bi. Tukuku.

> **"Tumezoea kutumia kuni na mkaa kwa sababu ya mazoea, lakini sasa nimeelewa hatari zake kiafya na kimazingira. Nitahakikisha nakuwa balozi mzuri wa elimu hii kwa familia yangu na majirani**

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Bw. Msakasozi Seiphu, alieleza namna elimu hiyo ilivyomfungua macho kuhusu madhara ya nishati chafu na faida za kutumia nishati salama.

"Tumezoea kutumia kuni na mkaa kwa sababu ya mazoea, lakini sasa nimeelewa hatari zake kiafya na kimazingira. Nitahakikisha nakuwa balozi mzuri wa elimu hii kwa familia yangu na majirani," alisema Bw. Seiphu.

Akihitimisha mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Tanga, ndugu Twali Mshare, alisisitiza umuhimu wa kuendelea kuwashirikisha vijana katika juhudi za kitaifa za kuhamasisha matumizi ya nishati safi, akisema:

"Vijana ndiyo nguvu kazi ya taifa. Tukiwajengea uelewa leo, tunaihakikishia nchi kesho yenye watumiaji wa huduma waliokomaa kifikra na walio tayari kulinda afya na mazingira yao."

Kupitia kampeni hiyo, EWURA CCC imeonesha kwa vitendo dhamira yake ya kuwa daraja kati ya watoa huduma na wananchi, kwa kuhakikisha elimu sahihi inafikia kila kundi, hasa vijana, ambao ni msingi wa mabadiliko ya kudumu katika jamii.



*Wanaklabu wa EWURA CCC Shule ya Sekondari Tanga wakielimisha umma kuhusu Baraza na majukumu yake wakati wa mahafali ya Kidato cha Sita yaliyofanyika Shuleni hapo hivi karibuni.*

# Changamoto ya maji Mateka "C" yahitaji ufumbuzi wa haraka

Na Magreth Temba, Ruvuma

Wakazi wa Mtaa wa Mateka C, Kata ya Mateka katika Manispaa ya Songea, wameeleza kwa masikitiko makubwa kero ya kukosa huduma ya majisafi na salama kwa zaidi ya siku saba mfululizo, hali inayowalazimu kutumia vyanzo visivyo salama vya maji kama visima na mito, na hivyo kuhatarisha afya zao.

Malalamiko hayo yaliwasilishwa moja kwa moja mbele ya Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Ruvuma (RCC Ruvuma), wakati wa kampeni ya utoaji elimu kwa umma kuhusu haki na wajibu wa watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na EWURA, iliyofanyika hivi karibuni katika eneo hilo.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Bw. Ally Mkilima, alisema licha ya kuwepo kwa miundombinu ya maji, huduma hiyo imekuwa ikikatika kwa muda mrefu bila maelezo ya kuridhisha kutoka kwa mtoa huduma.

"Miundombinu ipo lakini hatupati maji. Tunatumia fedha nyingi kununua maji, wakati tayari tunalipia ankara kila mwezi. Hatuelewi kwa nini hali hii iendelee, hasa tukizingatia usalama wa maji tunayoyatumia kutoka vyanzo vya asili ni wa mashaka," alisema Bw. Mkilima.

Akielezea kwa uchungu athari za ukosefu wa maji kwa akina mama, Bi. Mary Komba, mkazi wa Mateka C, alisema ukosefu wa maji unaathiri majukumu ya familia moja kwa moja.

"Tulishaahidiwa kuwa tatizo litashughulikiwa, lakini bado hali ni ileile. Sisi akina mama tunaumia zaidi kwa sababu maji ni kila kitu kwenye familia," alisema.

Baada ya kusikiliza changamoto hizo, EWURA CCC Mkoa wa Ruvuma ilichukua hatua ya kuwasiliana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) ili kupata maelezo na hatua zinazochukuliwa kutatua tatizo hilo.

Afisa Uhusiano wa SOUWASA, Bw. Paul Mandia, alifafanua kuwa eneo la Mateka C liko kwenye miinuko, hivyo linakumbwa na changamoto za kimazingira na kiufundi kutokana na kutumia miundombinu ya zamani ya usambazaji maji.

"Kwa sasa tunazalisha lita milioni 11.5 za maji kwa siku dhidi ya mahitaji ya lita milioni 21.78 kwa Manispaa nzima. Hali hii imesababishwa pia na ongezeko la watu. Tuna matumaini kuwa changamoto hii itapatiwa suluhisho la kudumu kupitia Mradi wa Maji wa Miji 28, unaotarajiwa kukamilika Septemba 2026," alisema Bw. Mandia.

Aidha, alieleza kuwa SOUWASA imeanza kutekeleza mikakati ya muda mfupi ikiwemo maboresho ya miundombinu midogo ya usambazaji ili kupunguza adha hiyo kwa wakazi wa maeneo ya miinuko kama Mateka C.

Kwa upande wake, EWURA CCC imeahidi kuendelea kufuatilia kwa karibu hatua zote zinazochukuliwa ili kuhakikisha wakazi wa eneo hilo wanapata huduma ya maji safi, salama na endelevu kama inavyostahili kisheria.

"Hili ni suala la haki ya msingi ya binadamu. Tunasisitiza kuwa kila mtoa huduma awajibike kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma bora na kwa wakati," alisema mmoja wa wajumbe wa RCC Ruvuma.

"Kwa sasa tunazalisha lita milioni 11.5 za maji kwa siku dhidi ya mahitaji ya lita milioni 21.78 kwa Manispaa nzima. Hali hii imesababishwa pia na ongezeko la watu. Tuna matumaini kuwa changamoto hii itapatiwa suluhisho la kudumu kupitia Mradi wa Maji wa Miji 28, unaotarajiwa kukamilika Septemba 2026






Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Tanga, Bi. Bertha Maqway, akimpatia kipeperushi, mmoja wa washiriki wa elimu kwa wanachama wa vikundi vya wanawake walemavu na Vijana, mjini Tanga

Makala

# Nishati safi ya kupikia: Ufunguo wa afya, maendeleo na hifadhi ya mazingira

Nuru Na Zuberi, Tanga na Zamda Mabada, Kilimanjaro

Katika familia nyingi za Kitanzania, moshi kutoka jikoni umekuwa sehemu ya maisha ya kila siku. Lakini nyuma ya moshi huo kuna hatari kubwa zinazoligharimu taifa kiafya, kimazingira na kijamii. Hii ndiyo sababu Serikali ya Tanzania, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo EWURA CCC, imeazimia kuleta mabadiliko ya kudumu kupitia matumizi ya nishati safi ya kupikia.

### Takwimu Zinasema Nini?

Kwa mujibu wa ripoti ya mwaka 2021 kuhusu hali ya matumizi ya nishati ya kupikia nchini Tanzania, ni asilimia 6.9 tu ya Watanzania waliokuwa wakitumia nishati safi ya kupikia kama gesi, umeme au bayogesi. Asilimia zaidi ya 90 walitegemea kuni na mkaa, huku vijijini hali ikiwa mbaya zaidi.

Athari zake ni kubwa zikijumuisha ukataji miti, magonjwa ya mfumo wa upumuaji, na ukosefu wa muda wa kujifunza au kufanya kazi kwa wanawake na watoto.

### Nishati Isiyo Salama: Gharama Zinazoumiza

Matumizi ya kuni na mkaa husababisha, maradhi kama pumu, saratani ya mapafu na vifo vya ghafla hasa kwa watoto wachanga.

Athari zingine ni pamoja na uharibifu mkubwa wa mazingira, ukataji wa misitu na mabadiliko ya tabianchi, muda mwingi kupotea kutafuta kuni badala ya kufanya kazi au kujifunza na hatari za kijinsia kwa wanawake wanaoingia misituni kutafuta kuni.

### Suluhisho: Nishati Safi ya Kupikia

Serikali kupitia Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2024–2034 inalenga kuhakikisha asilimia 80 ya kaya nchini zinatumia nishati safi ifikapo mwaka 2034. Aina kuu za nishati safi ni pamoja na:

- Umeme (EPCs/Induction): Hakuna moshi, huokoa muda na salama.
- Bayogesi: Huzalishwa kwa mabaki ya mimea na samadi, nafuu na rafiki kwa mazingira.
- LPG/Gesi Asilia: Inawaka haraka, salama, na rafiki wa mazingira.
- Mkaa Mbadala (Briquettes/Pellets): Unazalishwa kwa mabaki ya mazao na hupunguza ukataji miti.

### EWURA CCC: Elimu kwa jamii

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limejikita katika kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi. Kupitia kampeni za uhamasishaji, mikutano, warsha na ushirikiano na wadau mbalimbali, Baraza limewafikia maelfu ya Watanzania, wengi wao wakiwa ni wanawake na vijana ili kuhamasisha mabadilika katika matumizi ya nishati ya kupikia.

Afisa kutoka EWURA CCC Tanga, Bi. Nuru Zuberi anasema “Mabadiliko haya hayawezi kutokea bila wananchi kuelimishwa kuhusu haki na wajibu wao. Tunawahamasisha kujua athari za nishati isiyo salama na faida za kutumia nishati safi ya kupikia kwa afya na mazingira.”

Aliongeza kuwa kwa kila kaya itakayohamia kwenye matumizi ya nishati safi, taifa linapiga hatua moja mbele katika kulinda misitu, kuboresha afya za wananchi, na kukuza uchumi wa familia. Hili si jukumu la serikali pekee, ni wajibu wa kila Mtanzania.

# Matangazo


DAWASA
Rafiki je
UMELIPA
Ankara yako ya Maji? Lipa sasa kwa kutumia Mitandao ya Simu na Benki washirika ambazo ni:
MITANDAO YA SIMU
airtel money
*150*60#
T-PESA
*150*71#
halopesa
*150*88#
tigo pesa
*150*01#
m-pesa
*150*00#
BENKI WASHIRIKA
NMB
NBC
Stanbic Bank
absa
CRDB BANK
Tanzania Commercial Bank
Azania Bank Ltd
dawasatz


WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI IRINGA (IRUWASA)
IRUWASA UPDATE
7/5/2025
MAENEO YENYE MILIMA
TRM JUU SASA MAJI NI MWAAA MWAAA!
0800110088
@iruwasa
www.iruwasa.go.tz


MORUWASA
Maliza Mwezi Kizalendo
KWA KULIPA BILI YAKO YA MAJI
KUEPUSHA MALIMBIKIZO NA KUSITISHIWA HUDUMA
Unaweza kulipa kupitia Mitandao ya Simu au Benki washirika
Mitandao ya Simu
Banki washirika
kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia namba
0800751011
(Bure)
"Maji ni Uhai, Tulipe bili kwa wakati kwa Huduma Bora na Endelevu"
moruwasa moruwasa2 moruwasamaji 0736737736 0800751011 Bure


WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MUSOMA
HUDUMA YA GARI LA
MAJITAKA
WASILIANA NASI KUPITIA
0800 110 108 (BURE)
0615791939 (WhatsApp tu)
au
Fika Kwenye Ofisi za MUWASA za eneo husika
@muwasamusoma
www.muwasa.go.tz


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TABORA (TUWASA)
NAMNA YA KUWASILISHA MALALAMIKO AU KUTOA TAARIFA TUWASA
Ndugu mteja, TUWASA inapokea na kushughulikia malalamiko kuhusu utoaji wa huduma. Mteja anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa kutumia njia zifuatazo
Fika katika Ofisi ya Huduma kwa Wateja (TUWASA)
Kuandika Barua pepe( maji@tuwasa.go.tz) au barua kwa Mkurugenzi Mtendaji
Kupiga simu Bure yenye nambari 0800780063
Kuweka kwenye makundi mbalimbali ya WhatsApp yaliyoanzishwa na Ofisi za TUWASA maeneo tofauti tofauti yakiwaunganisha Wateja wanaoishi katika eneo Husika
TUWASA kwa Majisafi na Salama
0800780063 tuwasatabora.3 tuwasa_tabora www.tuwasa.go.tz


TANESCO
UNAWEZA KUONA TOKEN ZAKO ZA UMEME KUPITIA GePG APP
Ndugu Mteja!
Endapo utakuwa umenunua umeme na haujapata token au umezifuta unaweza kuziona kwa kupitia GePG App
KUONA UMEME WAKO ULIONUNUA FATA TARATIBU ZIFUATAZO
1. Pakua GePG App
2. Ingia kwenye menu ya GePG kwenye simu yako
3. Chagua LUKU
4. Chagua get last token ( ona umeme wa mwisho)
5. Chagua unataka kuona kwa kutumia namba ya simu uliyonunulia umeme au Namba ya Mita au Namba ya risiti
6. Ingiza namba ya mita au namba ya simu au namba ya risiti
7. Bofya Wasilisha ( Submit)
8. Token za umeme wako ulizonunua hivi karibuni zitaonekana
9. Bofya mshale wa token husika kuone maelezo zaidi (Umenuna lini, kiasi, token husika nk)
www.tanesco.co.tz

# Safari ya haki: Bi. Husna aondokana na deni bandia kwa msaada wa Baraza

Na Nuru Zuberi, Tanga

Alipoambiwa deni lake la maji limefikia zaidi ya shilingi milioni mbili na laki sita, Bi. Husna Ngoda mkazi wa Magaoni, Tanga, aliduwaa. Hakuwa na jibu. Hakuwa na njia. Na zaidi ya yote, alisitishiwa huduma hiyo ya maji.

Kwa mwaka mzima, aliishi na mzigo wa deni la shilingi 2,675,104 ambalo si tu kwamba halikuwa la kweli kulingana na matumizi yake, bali pia lilimfungia nje ya huduma ya msingi ya maji. Kilichomsikitisha zaidi ni kuwa hakuwa na uelewa wala msaada wa kumwelekeza pa kuanzia. Alihangaika na kubeba mzigo huo kimyakimya.

Lakini siku moja, kupitia kipindi cha redio cha Mseto kilichorushwa na Nuur FM tarehe 1 Novemba 2022, aliguswa na ujumbe uliokuwa ukitolewa na EWURA CCC, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji. Kupitia kipindi hicho alisikia kuwa mtumiaji wa huduma za maji ana haki ya kulipa bili halali za matumizi ya huduma za maji, na sio bili zisizoakisi matumizi halisi ya mtumiaji.

Tumaini jipya kwa Bi. Husna.

"Nilikuwa nimekata tamaa, lakini niliposikia kuhusu haki za mtumiaji zilizokuwa zikielezwa na EWURA CCC, nikapata tumaini jipya. Nilipiga simu EWURA CCC na walinisikiliza kwa upendo. Wakanishauri na kuanza kufuatilia suala langu," anasimulia Bi. Husna.

Ndani ya wiki mbili tu baada ya kuwasiliana na EWURA CCC, Bi. Husna akaitwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Tanga (Tanga UWASA) na kupewa taarifa mpya, kuwa deni lake lilipunguzwa kutoka shilingi milioni mbili na zaidi hadi shilingi 144,000 tu.

"Asikwambie mtu nililia kwa furaha. Sikuamini kilichotokea. Nilihisi kama mzigo mkubwa umeondolewa kichwani mwangu," anasema Bi. Husna akiwa bado na msisimko wa tukio hilo.

Tukio hilo halikuwa la bahati tu. EWURA CCC ilifuata utaratibu kwa umakini na weledi. Bi. Husna alishauriwa kujaza fomu rasmi ya malalamiko kwenda EWURA, huku EWURA CCC ikifuatilia suala hilo kwa karibu. Uchunguzi wa pamoja kati ya EWURA CCC na Tanga UWASA, ulionesha kulikuwa na hitilafu kubwa katika mfumo wa kielektroniki wa kuchakata bili za maji. Mfumo huo ulikuwa umezalisha makosa ya kimahesabu yaliyosababisha deni bandia.

"Naishukuru sana EWURA CCC. Wameniondolea mzigo mkubwa sana wa kiakili, kifedha, na kihisia. Nawahamasisha wanawake wote na jamii kwa ujumla kwamba msinyamaze mkiona hamjatendewa haki.

Baada ya marekebisho, ukweli ulijulikana. Deni halali lilikuwa ni shilingi laki moja na kidogo tu. EWURA CCC ilihakikisha kwamba haki inapatikana, na huduma ya maji kurejeshwa haraka.

"Naishukuru sana EWURA CCC. Wameniondolea mzigo mkubwa sana wa kiakili, kifedha, na kihisia. Nawahamasisha wanawake wote na jamii kwa ujumla kwamba msinyamaze mkiona hamjatendewa haki. Itumieni EWURA CCC kwani wanasaidia bure kabisa," anasisitiza Bi. Husna.

Ushuhuda huu wa Bi. Husna ni zaidi ya simulizi ya mtu mmoja. Ni ushahidi hai wa dhima ya EWURA CCC kama nguzo ya utetezi kwa watumiaji wa huduma muhimu. Ni somo kwa jamii kwamba pale ambapo sauti ya mwananchi inaimarishwa kwa maarifa sahihi, suluhu huwezekana!

Usinyamaze unapoumia

Kama unaona hujatendewa haki katika huduma za maji, umeme, gesi asilia au mafuta, usikate tamaa. Anza kwa kuwasiliana na mtoa huduma wako. Lakini endapo huoni mwanga, mwelekeo au msaada, jua kuwa EWURA CCC ipo kwa ajili yako. Watakushauri, watakutetea, na watafuatilia hadi haki yako ipatikane, na yote haya hufanyika bure kabisa!



# Wananchi wapaza sauti: 'Tunahitaji gesi karibu nasi'

**Na. Zamda Mabada, Kilimanjaro**

Wakazi wa Kata ya Kirua Vunjo Kusini, mkoani Kilimanjaro, wameomba serikali kuhamasisha uwekezaji wa vituo vya usambazaji wa gesi ya kupikia katika maeneo ya vijijini, ili kuwapunguzia adha ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Ombi hilo limetolewa na wakazi wa Kijiji cha Kirua wakati wa programu ya utoaji elimu kwa wananchi iliyoandaliwa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), iliyofanyika hivi karibuni.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Kirua Vunjo Kusini, Ndugu Hassani Msheri, alisema kuwa pamoja na juhudi za Serikali kusambaza mitungi ya gesi kupitia makampuni mbalimbali, changamoto kubwa inayowakabili ni ukosefu wa mawakala wa kuuza na kubadilisha gesi hiyo.

"Tunaishukuru serikali kwa kushirikiana na kampuni za gesi kusambaza mitungi kwa wananchi katika jitihada za kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Hata hivyo, bado tunakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mawakala hapa kijijini, jambo linalotulazimu kutumia gharama kubwa kwenda mbali kufuata gesi," alisema Bw. Msheri.

Kwa upande wake, Bw. Kiswigu Swillah, Afisa Mtendaji wa Kata ya Kirua Vunjo Kusini, alisema kuwa, ukosefu wa mawakala wa gesi unalazimu wakazi wa kata hiyo kusafiri hadi mjini kwa ajili ya huduma hiyo, hali inayowaathiri kiuchumi.

"Kwa sasa hatuna mawakala wa kuuza au kubadilisha mitungi ya gesi, kwa baadhi ya makampuni ya gesi. Tunalazimika kwenda mjini, jambo ambalo linatuongezea gharama za usafirishaji. Hii hali ikiendelea, huenda baadhi wakarudi kutumia kuni, hali itakayoharibu jitihada za serikali za kulinda afya za wananchi na kuhifadhi mazingira kupitia matumizi ya nishati safi ya kupikia," aliongeza Swillah.

Aidha, Swillah alitoa wito kwa serikali na wadau wa nishati safi kuchukua hatua za haraka kuhakikisha mawakala wa gesi wanapatikana vijijini, akisisitiza kuwa ni haki ya kila mtumiaji kupata huduma bora na ya uhakika.

Akijibu kuhusu changamoto hiyo, Bw. Haleluyah Raymond Kagero, Meneja wa Maendeleo ya Biashara wa Kampuni ya Lake Energy (Kanda ya Kaskazini), alikiri kupokea malalamiko hayo kupitia ofisi za EWURA CCC Mkoa wa Kilimanjaro.

Kagero alieleza kuwa kampuni hiyo tayari imesambaza mitungi zaidi ya 500 ya gesi yenye ujazo wa kilo 6 kwa vijiji sita vya kata hiyo kupitia mradi wa REA, vikiwemo vijiji vya Mabungo, Uchira, Koresa, Yamu Makaa, Yamu na Uparo.

"Tumepokea changamoto hii na tumeona pia ipo maeneo mengine. Tumejipanga kutembelea vijiji tulivyosambaza mitungi ili kuangalia uwezekano wa kupata mawakala miongoni mwao," alisema Kagero.

Aliongeza kuwa mkakati wa kampuni yao pia ni kusambaza mitungi mikubwa ya kilo 15 katika maeneo mengine ya mkoa wa Kilimanjaro, ikiwa ni pamoja na kuanzia kwenye magereza ya mkoa huo ambako wanatarajia kugawa mitungi 510 yenye majiko ya sahani mbili.

Kwa upande mwingine, EWURA CCC Mkoa wa Kilimanjaro imesisitiza kuwa itaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa mijini na vijijini kuhusu matumizi salama na endelevu ya nishati safi ya kupikia kwa kuwa bado kuna uhitaji mkubwa wa uelewa miongoni mwa wananchi ili kusaidia kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, na hivyo kulinda afya na mazingira.




*Mitungi mbalimbali ya gesi za kupikia majumbani ikiwa ni hitaji muhimu kwa wakazi wa mijini na majumbani ili kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia.*

# Katizo la umeme Iringa kutatuliwa, Baraza laingilia kati

**Na Mwandishi Wetu, Iringa**

Kukatika kwa umeme mara kwa mara katika maeneo ya Ifunda, Ilula, Ipogolo na Pawaga mkoani Iringa kumeibua malalamiko mengi kutoka kwa wananchi, hali iliyolazimu Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kuingilia kati na kulishauri Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuchukua hatua madhubuti ili kurejesha huduma ya uhakika kwa wananchi.

Wananchi wamekuwa wakilalamikia kukosekana kwa huduma ya umeme wa uhakika kwa muda mrefu, jambo linaloathiri shughuli zao za kila siku, ikiwemo kilimo, biashara ndogondogo na uzalishaji wa viwandani.

Mmoja wa wakazi wa Pawaga, Bw. Lucas Ndete, ambaye ni mkulima na mfanyabiashara, alielezea namna tatizo hilo lilivyomgharimu kibiashara.

"Nilipoteza wateja kutoka Kenya waliokuja kununua mchele. Waliamua kuondoka kwa kuhofia hasara kwa kuwa mashine za kupakia na kupima hazikuweza kufanya kazi. Huu ni mzigo mkubwa kwa sisi wakulima," alisema kwa uchungu.

Kutokana na hali hiyo, hivi karibuni, EWURA CCC Mkoa wa Iringa ilifanya kikao cha dharura na uongozi wa TANESCO, Mkoa wa Iringa kwa lengo la kusikiliza upande wa mtoa huduma na kutafuta suluhisho la haraka.

Akizungumza wakati kikao hicho, Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Iringa, Bw. Painetho Madembwe, alisema kuwa changamoto hiyo imedhoofisha ustawi wa wananchi na kuhujumu juhudi za serikali za kukuza uchumi kupitia sekta ya nishati.

"Kutopatikana kwa umeme kumevuruga shughuli nyingi za wananchi, hasa walioko vijijini wanaotegemea mashine kwa ajili ya kilimo na viwanda vidogo. Ni hali inayokatisha tamaa," alisema.

Kwa upande wa TANESCO, Mhandisi Helman Bucheye, Kaimu Meneja wa Shirika hilo mkoani Iringa, alikiri kuwepo kwa changamoto hiyo, akieleza kuwa baadhi ya maeneo yanakumbwa na matatizo ya kiufundi, upungufu wa vifaa na uharibifu wa miundombinu.

> **"Tuna changamoto ya wizi wa vifaa vya umeme na uchomaji wa nguzo, hasa maeneo ya Ilula. Wananchi wanapaswa kushiriki kulinda miundombinu kwa sababu uharibifu huu unaathiri huduma kwa wote**

"Tuna changamoto ya wizi wa vifaa vya umeme na uchomaji wa nguzo, hasa maeneo ya Ilula. Wananchi wanapaswa kushiriki kulinda miundombinu kwa sababu uharibifu huu unaathiri huduma kwa wote," alisema Mhandisi Bucheye.

Aliongeza kuwa, TANESCO inaendelea kuboresha huduma kwa kushirikiana na wadau, huku akiahidi kuwa baadhi ya maeneo tayari yameanza kupangiwa matengenezo ya dharura ili kurejesha huduma.

Katika kikao hicho, pande zote mbili zilikubaliana kuimarisha ushirikiano na kuanzisha kampeni za kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya umeme, pamoja na ulinzi wa miundombinu ili kupunguza matukio ya uharibifu.

EWURA CCC imeahidi kuendelea kufuatilia utekelezaji wa maazimio hayo kwa karibu, huku ikiwasihi wananchi kuwasilisha malalamiko yao kwa njia rasmi ili yafanyiwe kazi kwa haraka.

"Baraza litaendelea kusimama na wananchi hadi pale huduma zitakaporejea kwa ubora na uhakika. Haki ya kupata umeme wa kuaminika siyo ombi, ni haki ya msingi," alisisitiza Bw. Madembwe.



# HabariPicha




Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Pwani ndugu Benjamin Ntigwambukwa (wa kwanza kushoto, akielimisha madereva wa bodaboda kuhusu haki na wajibu wa watumiaji wa huduma, katika kituo cha Daladala Mailimoja.



Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Mwanza Bi. Veronica Kageba, akielimisha wajasiriamali kuhusu majukumu ya Baraza, haki na wajibu wa watumiaji wa huduma za nishati na maji, pamoja na mchakato wa namna ya kuwasilisha malalamiko.



Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Manyara Bw. Deogratius Gallus, akielimisha wananchi wa Kijiji cha Gichameda, Wilayani Babati kuhusu majukumu ya Baraza wakati wa mkutano wa wananchi wa Kijiji hicho.




*Mkuu wa Mkoa wa Mara, Mhe. Kanali Evans Alfred Mtambi (kushoto aliyeshika kipaza sauti), akiuliza swali alipotembelea banda la EWURA CCC wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini yaliyoandaliwa na Mahakama Kuu ya Tanzania na kufanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Mukendo, mjini Musoma.*



*Afisa Mwandamizi Huduma kwa Wateja EWURA CCC Tanga, Bi. Nuru Zuberi Akielimisha wananchi kuhusu Baraza na kazi zake wakati wa mkutano wa Wananchi wa Mtaa wa Nguvumali Ikulu, jijini Tanga.*



*Afisa wa Huduma kwa Wateja EWURA CCC Iringa, Bi. Brenda Magoma (aliyevaa tisheti ya buluu), akieleza kuhusu kazi na majukumu ya Baraza kwa mmoja wa watumiaji wa huduma za nishati na maji aliyetembelea banda la EWURA CCC wakati wa Maonesho ya Ubunifu yaliyoandaliwa na Chuo Kikuu cha Iringa.*

# Wahimizwa matumizi sahihi ya maji misikitini

**Na Mwandishi wetu, Dodoma**

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limewahimiza wanafunzi wa Madrasa ya Bweni iliyopo Kata ya Ndachi, jijini Dodoma, kuzingatia matumizi sahihi ya maji katika maeneo ya ibada, ili kupunguza gharama na upotevu wa maji unaosababisha mzigo mkubwa kwa taasisi hizo.

Akizungumza katika ziara ya utoaji elimu ya matumizi ya huduma za maji, Afisa Huduma kwa Wateja Mwandamizi kutoka EWURA CCC Mkoa wa Dodoma, Bw. Amani Mbogo, alisema kuwa matumizi holela ya maji misikitini, hasa wakati wa kuchukua udhu, yamesababisha kuongezeka kwa bili ambazo zingetumika kuboresha huduma nyingine.

"Tumearifiwa kuwa baadhi ya wanafunzi huacha mabomba yakiwa wazi baada ya kuchukua udhu. Tabia hii husababisha upotevu mkubwa wa maji na gharama zisizokuwa za lazima kwa uongozi wa misikiti. Tunawasihi mjenge mazoea ya kufunga bomba kila mara baada ya matumizi," alisema Bw. Mbogo.

Aidha, aliwakumbusha wanafunzi kuwa matumizi sahihi ya maji yanapaswa kuzingatiwa pia katika shughuli nyingine kama kufua nguo na usafi wa mazingira.

"Unapofua, badala ya kutumia bomba moja kwa moja, tumia ndoo au beseni ili kupunguza matumizi ya maji. Ni njia bora ya kuokoa rasilimali hii muhimu," alisisitiza.


> **Tumejifunza mambo mengi leo. Nitahakikisha baba na mama wanajua umuhimu wa kuziba bomba na kutotiririsha maji hovyo**

Kwa upande wao, baadhi ya wanafunzi walieleza kufurahishwa na elimu waliyoipata, wakiahidi kuwa mabalozi wa matumizi salama ya maji katika familia zao.

"Tumejifunza mambo mengi leo. Nitahakikisha baba na mama wanajua umuhimu wa kuziba bomba na kutotiririsha maji hovyo," alisema mwanafunzi Haji Said.

Kampeni hiyo ya uhamasishaji ni sehemu ya juhudi za EWURA CCC kuelimisha wananchi, hususan kwenye misikiti kuhusu haki, wajibu na matumizi salama ya huduma za nishati na maji. Baraza limekuwa likishirikiana kwa karibu na viongozi wa dini na serikali za mitaa ili kutekeleza jukumu hili.

Jitihada hizi zimefuatia kibali rasmi kilichotolewa na Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Mustapha Rajabu Shabani, kinachoruhusu Baraza kutoa elimu hiyo kwa waumini wa Kiislamu katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma.





*Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC Kagera Bi. Anadorice Komba, akielimisha juu ya kazi za Baraza pamoja na kusisitiza umuhimu wa wananchi kutoa taarifa za mivujo katika mkutano wa Mtaa wa Bugambakamo uliopo Bukoba Mjini.*

# Toeni taarifa za mivujo

**Na Mwandishi wetu, Kagera**

Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoa wa Kagera imewataka watumiaji wa huduma za maji kujenga tabia ya kutoa taarifa za mivujo mara moja wanapobaini matatizo hayo, ili kupunguza upotevu wa maji na kuleta manufaa kwa pande zote, yaani watumiaji na watoa huduma.

Kauli hiyo ilitolewa na Bi. Anadorice Komba, Afisa Huduma kwa Wateja wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoa wa Kagera, wakati wa mkutano wa uelimishaji uliofanyika Februari 2025 katika Mtaa wa National Housing, Kata ya Rwamishenye, Manispaa ya Bukoba.

Bi. Komba aliwasisitiza wakazi wa eneo hilo kutoa taarifa haraka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba (BUWASA) au uongozi wa mtaa pale panapobainika bomba limepasuka au kuna mivujo yoyote ili kupunguza upotevu wa maji.

"Upotevu wa maji unaosababishwa na mivujo huongeza gharama za uzalishaji, na gharama hizi huathiri moja kwa moja bei ya maji kwa watumiaji. Ni muhimu kwa kila mtumiaji kuwa makini na kutoa taarifa mara moja pindi anapogundua mivujo," alisema Bi. Komba.

Aliongeza kuwa, kulingana na Taarifa ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa mwaka wa fedha 2023/2024, upotevu wa maji kwa BUWASA ni asilimia 36, kiwango kinachozidi kiwango kinachokubalika cha asilimia 20 kilichowekwa na EWURA. Aidha, alisisitiza kuwa kutoa taarifa kuhusu hali ya upatikanaji wa huduma ni moja ya wajibu muhimu wa watumiaji.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa National Housing, Bw. David Dominick, aliomba BUWASA kushughulikia taarifa za mivujo kwa haraka zaidi, akisisitiza kuwa ucheleweshaji umesababisha kuendelea kwa upotevu wa maji na kuleta kukata tamaa kwa wananchi wanaotoa taarifa.

"Mamlaka iweke namba za simu za simu za kupiga bila malipo katika ofisi za serikali za mitaa ili kuwawezesha wananchi kutoa taarifa za haraka na hivyo kupunguza tatizo hili," aliomba Bw. Dominick.

Kwa kuzingatia changamoto hizo, ofisi ya Baraza mkoani Kagera ilifanya kikao na uongozi wa BUWASA kwa lengo la kutafuta suluhisho la haraka na endelevu.

Akizungumzia hatua zinazochukuliwa, Meneja Huduma kwa Wateja wa BUWASA, Bw. Deogratius Setse, alisema kuwa kukabiliana na upotevu wa maji kunazingatiwa kwa makini kwa sababu gharama kubwa hutumika kulipia umeme na dawa za kutibu maji ambazo hupotea kutokana na mivujo.

"Tunaendelea na mradi wa kubadilisha mabomba ya chuma yaliyokaribia kuharibika na kuweka mabomba ya plastiki katika kata nne za Manispaa ya Bukoba, hatua inayotarajiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa upotevu wa maji," alisema Bw. Setse.

Pia aliwataka watumiaji kuwa mabalozi wazuri kwa kutoa taarifa za mivujo badala ya kuwa chanzo cha upotevu wa maji kwa kukata mabomba bila ruhusa.

Kwa urahisi wa kutoa taarifa, Bw. Setse aliwataka wananchi kutumia namba ya simu ya bure 0800712080 kwa ajili ya kuripoti mivujo au changamoto nyingine zinazohusu huduma za maji.

# Matumizi salama ya umeme: Jukumu la kila mtumiaji

**Na Noela Ntiluvakule, Pwani**

Nishati ya umeme ni chachu muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania. Huduma hii imewezesha uendeshaji wa viwanda, biashara, taasisi, kilimo na kuboresha maisha ya watu majumbani. Hata hivyo, matumizi yasiyo salama ya umeme yameendelea kuwa chanzo cha ajali, moto, uharibifu wa mali, vifo na hasara kubwa kwa familia na biashara.

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), kupitia programu zake za elimu kwa umma, linaendelea kuhimiza matumizi salama na ya tahadhari ya umeme.

Kwa mujibu wa Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 na Kanuni za Umeme za mwaka 2022, kila mtumiaji ana wajibu wa kuhakikisha matumizi ya umeme yanafanyika kwa kufuata taratibu salama ili kulinda maisha na mali.

### Nini cha kuzingatia? Tumia mafundi walioidhinishwa

Miongoni mwa vyanzo vikuu vya ajali za umeme ni uunganishaji holela wa miundombinu ya umeme unaofanywa na mafundi wasio na sifa. Kanuni ya 15(1) ya Kanuni za Umeme (2022) inasisitiza kuwa kazi yoyote ya ufungaji wa mifumo ya umeme lazima ifanywe na mkandarasi au fundi mwenye leseni ya EWURA.

Kanuni ya 19(1) na (2) ya Kanuni tajwa hapo juu pia inamtaka mmiliki wa jengo kuhakikisha mkandarasi anayefanya kazi ana leseni halali, na mfumo huo unakaguliwa kila inapohitajika. Hii inalenga kupunguza ajali, kulinda vifaa na kuimarisha ubora wa huduma ya umeme.

### Tahadhari muhimu za kuepuka ajali

Kwa kuzingatia miongozo ya kitaalamu kutoka TANESCO, EWURA CCC inashauri hatua zifuatazo kuchukuliwa na kila mtumiaji wa umeme:

- Epuka kuchoma moto karibu na nyaya au nguzo za umeme kwani moto unaweza kusababisha mlipuko au kukatika kwa umeme.
- Usifanye shughuli za kibiashara chini ya transfoma, kwani ni maeneo hatarishi yenye mkondo mkubwa wa umeme.
- Usiguse wala kuchezea waya wa kuimarisha nguzo (stay wire) kwani ukivutika unaweza kusababisha nguzo kuanguka.
- Usikate miti karibu na nyaya za umeme bila ushauri wa TANESCO.
- Usiguse waya wa umeme ulioanguka – toa taarifa mara moja kwa TANESCO au EWURA CCC.

> **Kwa mujibu wa Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 na Kanuni za Umeme za mwaka 2022, kila mtumiaji ana wajibu wa kuhakikisha matumizi ya umeme yanafanyika kwa kufuata taratibu salama ili kulinda maisha na mali.**

### Mchango wa EWURA CCC katika elimu ya usalama wa umeme

EWURA CCC inaendelea kushirikiana na TANESCO kuelimisha wananchi kupitia vipindi vya redio, mitandao ya kijamii, vipeperushi, na mikutano ya ana kwa ana. Lengo ni kuhakikisha kila mtumiaji anatambua haki, wajibu na hatua stahiki za kuchukua pale panapotokea changamoto au hitilafu ya umeme.

Kwa kuzingatia mafunzo haya, tunahimiza wananchi wote kuwa mabalozi wa matumizi salama ya umeme katika jamii zao. Umeme ni muhimu, lakini usipotumika kwa uangalifu unaweza kuleta hatari kubwa.








*Waandishi wa habari Mkoa wa Dodoma wakipata elimu kuhusu utaratibu wa kuwasilisha malalamiko kupitia Baraza. Elimu hiyo ilitolewa hivi karibuni na Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Dodoma, Bi. Dotto Kwilasa (hayupo pichani).*

# Waandishi wa habari daraja kuu la mawasiliano: EWURA CCC

**Na Amani Mbogo, Dodoma**

Waandishi wa habari mkoani Dodoma wametakiwa kutumia majukwaa yao ya habari kusaidia kuwaelimisha wananchi kuhusu haki na wajibu wao katika kupata huduma bora za nishati na maji, ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kuwasilisha malalamiko kupitia Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC).

Wito huo umetolewa wakati wa kikao na waandishi wa Habari, kilichofanyika katika ukumbi wa Idara ya Habari – Maelezo jijini Dodoma, na kuwahusisha waandishi kutoka vyombo mbalimbali vya habari.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma Mkoa wa Dodoma, Bi. Dotto Kwilasa, alisema kuwa waandishi wa habari ni daraja muhimu kati ya wananchi na watoa huduma, hivyo wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kueneza elimu kuhusu matumizi salama, sahihi na yenye ufanisi ya huduma zinazodhibitiwa na EWURA.

"Wananchi wengi bado hawajui kuwa wana haki ya kuwa na mkataba wa huduma kutoka kwa watoa huduma kama TANESCO au mamlaka za maji. Wengine hawajui kuwa wanaweza kupeleka malalamiko yao kwa watoa huduma au EWURA CCC bila gharama yoyote. Ninyi waandishi mnaweza kubadili hali hii kupitia habari zenu," alisema Bi. Kwilasa.

> **"Kabla ya kikao hiki, wengi wetu tulikuwa hatufahamu vizuri majukumu ya EWURA CCC. Sasa tumepata mwanga wa kutosha na tuko tayari kuwa mabalozi wa Baraza kupitia kazi zetu za kila siku**

Aliongeza kuwa mchango wa vyombo vya habari ni wa kipekee katika kuongeza uwajibikaji wa watoa huduma na kuwawezesha wananchi kutumia sauti yao kudai huduma stahiki.

Kwa upande wao, baadhi ya waandishi wa habari walioshiriki kikao hicho walipongeza EWURA CCC kwa kuwahusisha katika mchakato wa kuelimisha jamii kuhusu haki za watumiaji, huku wakiahidi kutumia kalamu zao kueneza elimu hiyo kwa umma.

"Kabla ya kikao hiki, wengi wetu tulikuwa hatufahamu vizuri majukumu ya EWURA CCC. Sasa tumepata mwanga wa kutosha na tuko tayari kuwa mabalozi wa Baraza kupitia kazi zetu za kila siku," alisema Bw. Salehe Mtemi, mmoja wa waandishi waliotoa mrejesho baada ya kikao.

EWURA CCC kupitia Kamati yake mkoani Dodoma, imesisitiza kuwa ushirikiano wa karibu na waandishi wa habari ni nguzo muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza, ikiwa ni pamoja na kuimarisha sauti ya wananchi na kudhibiti changamoto katika upatikanaji wa huduma bora, salama na endelevu za nishati na maji nchini.

# Jaji Mruma: Ushiriki wa EWURA CCC katika majukwaa ya sheria ni wa kuigwa

Na Chipegwa Samwel, Morogoro

Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro, Mheshimiwa Amiri Mruma, amelipongeza Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kwa namna linavyoshiriki kikamilifu katika majukwaa ya kisheria kwa lengo la kuwaelimisha wananchi kuhusu haki na wajibu wao katika kupata huduma bora za nishati na maji.

Akizungumza katika hafla ya kufunga maonesho ya wiki ya kisheria yaliyofanyika jijini Morogoro, Jaji Mruma alieleza kuwa, ushiriki wa taasisi kama EWURA CCC ni wa kuigwa kwani husaidia kuondoa uelewa hafifu wa wananchi kuhusu haki zao za kisheria, hususan katika mazingira ya huduma duni.

"Wananchi wengi bado hawajui haki zao. Hata wasomi wapo ambao hawajui wanapaswa kufanya nini wanapopata huduma duni kama kukatika kwa umeme au bili kubwa isiyoeleweka. Hii si hali ya kuzoeleka, tunahitaji kuelimisha umma ili wajue namna ya kudai fidia au kufuatilia haki zao kwa mujibu wa sheria," alisisitiza Jaji Mruma.

Alisema kuwa Mahakama inapaswa kushirikiana kwa karibu na wadau wa udhibiti kama EWURA pamoja na mabaraza ya watumiaji ili kuendeleza juhudi za kuwafikishia wananchi elimu ya sheria kwa njia nyepesi na ya moja kwa moja.

Katika maonesho hayo, EWURA CCC kupitia Kamati ya Watumiaji Mkoa wa Morogoro ilitoa elimu kwa wananchi kuhusu haki zao kisheria dhidi ya watoa huduma, jinsi ya kuwasilisha malalamiko, na wajibu wao katika utunzaji wa miundombinu ya huduma. Elimu hiyo ilitolewa kwa njia ya mazungumzo ya moja kwa moja, vipeperushi, na majadiliano ya vikundi.

Katibu wa Kamati hiyo, ndugu Daudi Eliya, alisema Baraza limejipanga kuhakikisha elimu ya matumizi sahihi na salama ya huduma za umeme, maji, gesi na mafuta inawafikia wananchi wengi kupitia majukwaa ya kitaifa kama haya.

"Ushiriki wetu kwenye maonesho ya kisheria si wa bahati mbaya, bali ni sehemu ya mkakati wa kuhakikisha kuwa haki za watumiaji hazikai vitabuni tu, bali zinaeleweka na kutekelezwa kwa vitendo," alisema Eliya.

Katika kipindi chote cha maonesho, Baraza lilihudumia wananchi wapatao 79 waliotembelea banda lake, likapokea na kufuatilia malalamiko mbalimbali kuhusu huduma zisizoridhisha kutoka kwa baadhi ya watoa huduma wa maji, umeme, na bidhaa za mafuta.

Ushiriki wa EWURA CCC kwenye majukwaa kama haya umetajwa kuwa kichocheo muhimu cha kuongeza uwajibikaji kwa watoa huduma na kuwezesha jamii kufuatilia huduma wanazopaswa kuzipata kwa mujibu wa sheria na miongozo ya nchi.









# Fahamu aina ya mita ya umeme unayotumia, pamoja na faida zake

Na Catherine Charles, Ilala

Katika dunia ya teknolojia tunayoishi sasa, upatikanaji wa umeme wa uhakika ni msingi wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), likiwa mhimili wa usambazaji wa nishati hiyo nchini, limeendelea kuimarisha mifumo ya kupima matumizi ya umeme kupitia aina mbalimbali za mita za kisasa ili kuhakikisha mtumiaji anapata urahisi wa kutumia huduma, huku Shirika likipata mapato yatakayofanya huduma iwe endelevu.

Wakati huohuo, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limekuwa mstari wa mbele katika kutoa hamasa na elimu ya matumizi sahihi ya nishati ikiwemo huduma za umeme ili kuwa na watumiaji wenye uelewa mkubwa wa masuala muhimu yanayohusu huduma zinazodhibitiwa na EWURA.

Katika kutekeleza jukumu hilo, EWURA CCC inakuletea makala kuhusu mita mbalimbali za umeme zinazotumiwa na TANESCO ili unapozichagua na kuzitumia uwe unafahamu namna zinazovyofanya kazi, faida pamoja na hasara zake.

Zifuatazo ni aina kuu za mita zinazotumika nchini pamoja na faida na changamoto zake:

## 1. Mita za LUKU (Prepaid Meters)

Aina hii ya mita ni maarufu zaidi miongoni mwa Watanzania. Mita hii humwezesha mtumiaji kununua umeme kulingana na mahitaji yake kwa wakati husika. Manunuzi hayo hufanyika kwa njia ya vocha (tokeni) na kuingiza kwenye mita kabla ya kutumia.

- **Faida:**
  - o Mteja anadhibiti matumizi yake na kuepuka madeni.
  - o Malipo hufanyika kabla ya matumizi, hivyo TANESCO hupata mapato kwa wakati.
  - o Rahisi kutumia na kupunguza malalamiko ya bili isiyo sahihi.
- **Matumizi**
  - o Makazi ya kawaida na biashara ndogo ndogo.
  - o Maeneo yenye wateja wengi wenye matumizi ya kawaida.
- **Changamoto:**
  - o Changamoto za kupata tokeni kwa wakati au matatizo ya mifumo ya malipo.
  - o Baadhi ya wateja hawajui kutumia vyema mifumo hii.
  - o Udanganyifu na wizi wa tokeni.

## 2. Mita za Postpaid (Conventional Meters)

Aina hii ya mita hufanya kazi kwa kupima matumizi ya umeme ya mteja kisha kutoa taarifa kwa TANESCO ambayo hutengeneza bili ya mwezi. Malipo hufanywa baada ya huduma kutolewa, yaani, mteja anatakiwa kulipa kiasi kilichotumika kwa kipindi kilichopita, kulingana na usomaji wa mita.

Kwa kawaida, mita hizi hutegemea usomaji wa mita (manual reading), ambapo watumishi wa TANESCO hutembelea wateja kuchukua takwimu za matumizi. Hizi ni mita zinazotumika kwenye taasisi, viwanda, na baadhi ya nyumba za makazi.

- **Faida**
  - o Inaruhusu matumizi kabla ya malipo, ambayo ni msaada kwa taasisi na viwanda.
  - o Mteja ana uhakika wa kutumia kwa uhuru kabla ya kulipa.
- **Matumizi**
  - o Viwanda, taasisi, na wateja wakubwa.
  - o Wateja wa makazi wenye matumizi makubwa.
- **Changamoto**
  - o Inaweza kusababisha deni endapo mteja atachelewa au kukwepa kulipa
  - o Inaweza kutokea makosa ya usomaji wa mita na kupelekea bili isiyo sahihi.

## 3. Mita za AMI (Advanced Metering Infrastructure)

Aina hizi za mita zina teknolojia ya kisasa zaidi yenye uwezo wa kuwasiliana kwa pande mbili (two-way communication) kati ya mita na kituo cha usimamizi wa TANESCO.

*Inaendelea Uk. 26*

# Fahamu aina ya mita ya umeme unayotumia, faida zake

*Inatoka Uk. 25*

Mita hizi huweza kusomwa kwa njia ya mbali na kutoa taarifa za matumizi ya umeme kwa wakati halisi, kutuma taarifa kuhusu hitilafu, kuonesha hali ya mfumo, na hata kuwasha au kuzima huduma kwa mbali. Pia huiwezesha TANESCO kuchanganua matumizi ya umeme kwa ufanisi zaidi.

- **Faida**
  - o Usomaji wa mita kwa wakati halisi (real-time).
  - o Udhibiti wa mita kwa mbali (kuzima/kuwasha).
  - o Kupunguza wizi na matumizi yasiyo halali.
- **Matumizi**
  - o Wateja wakubwa, viwanda, na maeneo yenye teknolojia ya kisasa.
  - o Huduma za usimamizi wa mtandao wa umeme.
- **Changamoto**
  - o Gharama kubwa za kuunganishwa pamoja na matengenezo yake.
  - o Mahitaji ya miundombinu ya mawasiliano ya kidijitali.
  - o Upatikanaji mdogo wa teknolojia kwa maeneo ya vijijini.

### 4. Mita za AMR (Automatic Meter Reading)

Aina hii ya mita ina teknolojia inayolenga kusoma mita za umeme kwa njia ya mbali badala ya kusoma kwa mkono. Hii inamaanisha mita inasomwa na mfumo wa kompyuta bila kufika eneo husika. AMR hutoa data ya matumizi ya umeme tu na haina uwezo mkubwa wa kudhibiti mita au kutoa taarifa zaidi za hali ya mita.

- **Faida**
  - o Usomaji wa mita kwa umbali bila kuhitaji kusafiri kwenda kwa mteja.
  - o Kupunguza makosa ya usomaji wa mkono.
- **Matumizi:**
  - o Wateja wa kati na baadhi ya maeneo ya mijini.
- **Changamoto**
  - o Haidhibiti mita au kuripoti matatizo ya mita kwa wakati halisi.
  - o Hutegemea mtandao wa mawasiliano wa uhakika.

### 5. Mita za Pamoja (Bulk Meters)

Aina hii ya mita huwekwa kwa ajili ya kupima matumizi ya kundi la watumiaji wa umeme walioko kwenye eneo moja, kama vile maghorofa, hosteli, au mabweni. Badala ya kila mteja kuwa na mita yake binafsi, mita moja hupima matumizi ya jumla, kisha gharama hugawanywa kwa kila mteja kwa kutumia mfumo mwingine wa ndani (sub-metering) au kwa makadirio. Mita hizi husimamiwa na wenye nyumba au kampuni za usimamizi.

- **Faida**
  - o Hupunguza gharama kwa kupima matumizi ya umeme kwa kundi kubwa kwa mita moja.
  - o Rahisi kusimamia kwa nyumba za pamoja na maghorofa.
- **Matumizi**
  - o Maghorofa, nyumba za kupanga, na maeneo yenye wateja wengi.
- **Changamoto**
  - o Ugawaji wa gharama unaweza kuleta migogoro kati ya wateja.
  - o Ugumu wa kugundua matumizi haramu au matatizo ya kila mteja.

### 6. Mita za Viwandani (Maximum Demand Meters)

Aina hii ya mita zilitengenezwa mahsusi kwa ajili ya kupima matumizi ya umeme katika mazingira ya viwanda au taasisi kubwa. Mbali na kupima matumizi ya kawaida ya nishati, mita hii pia hupima kiasi kikubwa zaidi cha umeme (demand peak) ambacho kimewahi kutumika katika kipindi fulani. Hii husaidia TANESCO kufahamu muda na kiwango cha kilele ili kupanga uzalishaji na usambazaji wa umeme kwa ufanisi.

- **Faida**
  - o Husaidia kudhibiti matumizi ya juu na kuboresha ufanisi wa viwanda.
  - o Kusaidia kupanga uzalishaji wa umeme.
- **Matumizi**
  - o Viwanda na taasisi kubwa zenye mahitaji makubwa ya umeme.
- **Changamoto**
  - o Gharama kubwa za kuunganishwa pamoja na matengenezo yake.
  - o Uhitaji wa ujuzi wa kiufundi wa hali ya juu.




### Hitimisho

Mita za umeme si tu vifaa vya kupimia matumizi, bali ni chombo muhimu katika kuhakikisha haki, uwazi na ufanisi katika usambazaji wa nishati nchini. Kadiri teknolojia inavyoendelea kubadilika, elimu kwa watumiaji inazidi kuwa hitaji la msingi. EWURA CCC imejidhatiti kuwafikia watanzania kupitia njia mbalimbali, ili kuhakikisha kila mwananchi anatambua haki, wajibu na namna bora ya kutumia umeme salama, kwa gharama halali na kwa maendeleo ya taifa letu.

# Hasara iliyogeuka Baraka: Baraza laandika historia Sumbawanga

**Na Mwandishi Wetu, Rukwa**

Wakazi wa Mtaa wa Majengo KKKT, Kata ya Mafulala katika Manispaa ya Sumbawanga, wamepata fidia ya jumla ya shilingi milioni mbili (2,000,000/=) kufuatia hasara waliyoipata baada ya vifaa vyao vya umeme kuungua kutokana na hitilafu ya umeme. Mafanikio haya ni matokeo ya juhudi za EWURA CCC katika kutetea haki za watumiaji wa huduma za nishati na maji zinazodhibitiwa na EWURA.

Tukio hilo lililotokea hivi karibuni katika mtaa huo liliwaacha waathirika wakikata tamaa baada ya juhudi zao binafsi kukosa matokeo chanya. Hata hivyo, kupitia usaidizi wa EWURA CCC, walisaidiwa kuandaa malalamiko rasmi na kuelekezwa namna ya kuyawasilisha kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), hatua iliyosaidia kuanzisha mchakato wa madai ya fidia ambao ulihitimishwa kwa mafanikio.

"Nilikuwa nimeshakata tamaa baada ya kuzungushwa sana na TANESCO, lakini kupitia EWURA CCC tulipata msaada wa karibu hadi leo tumepata haki yetu," alisema Ndugu Elias Limbe, mmoja wa waathirika wa tukio hilo.

Aliongeza kuwa msaada wa Baraza haukuishia kwenye ushauri tu, bali ulihusisha pia kujaza fomu za malalamiko na kufuatilia mwenendo wa kesi yao hadi walipopokea fidia.

Kwa upande wake, Bi Stella Michael, ambaye alipoteza televisheni na kisimbuzi, alisema kuwa uzoefu wake wa mara ya kwanza na EWURA CCC ulimfundisha kuwa wananchi wana chombo halali cha kuwatetea.

"Sikuwahi kufikiria kama ningeweza kulipwa fidia, lakini leo hii nimeamini kuwa EWURA CCC ipo kwa ajili yetu watumiaji wa kawaida. Nawashukuru kwa kutusimamia," alisema Bi Michael.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Majengo KKKT, Bw. Pastory Helandogo, ambaye pia aliathirika na hitilafu hiyo ya umeme, aliishukuru EWURA CCC kwa kutoa elimu muhimu juu ya haki na wajibu wa mtumiaji wa huduma za nishati na maji.

"Kupitia EWURA CCC nimetambua haki na wajibu wangu. Elimu hii nitaipeleka kwa wananchi ninaowaongoza ili nao wajue namna ya kujitetea wanapoathiriwa," alisema Bw. Helandogo.

Waathirika hao kwa pamoja waliipongeza EWURA CCC si tu kwa kuwaongoza hatua kwa hatua katika kudai fidia, bali pia kwa kuwapa maarifa yatakayowasaidia kujiendesha kisheria katika siku zijazo. Wameahidi kuwa mabalozi wa EWURA CCC katika jamii yao kwa kueneza elimu ya utetezi wa haki za watumiaji wa huduma.




*Baadhi ya wananchi wa Mtaa wa Majengo KKT, Kata ya Mafulala, Manispaa ya Sumbawanga wakiwa nje ya ofisi ya EWURA CCC Rukwa, baada ya kupokea malipo ya fidia kutoka kwa TANESCO kufuatia uharibifu wa mali zao uliotokana na hitilafu ya umeme.*

# HabariPicha



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Iringa, ndugu Miraji Vanginothi akiwaelimisha Askari wa Jeshi la Polisi wa Mkoa wa Iringa kuhusu matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji.*



*Afisa Huduma kwa Wateja EWURA CCC Tabora, Bi. Sakina Yusuf akielimisha wanafunzi wa Shule ya Sekondari Cheyo kuhusu matumizi sahihi na salama ya huduma za nishati na maji.*



*Afisa Mwandamizi Huduma kwa Wateja EWURA CCC Kilimanjaro, Bi Zamda Mabada akiemisha walimu wa Shule ya Sekondari Kiboriloni iliyopo Manispaa ya Moshi kuhusu utaratibu wa kuwasilisha malalamiko kwa watoa huduma.*

# HabariPicha



*Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Kigoma, Bi. Rose Kanango (wa kwanza kushoto) akielimisha kuhusu EWURA CCC na kazi zake katika soko la dagaa la Rasini Kibirizi.*



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Kagera Bw. Lenas Katabazi akielimisha kuhusu kazi za Baraza kwa walimu na wanafunzi wa Shule ya Wasichana Rugambwa iliyopo Bukoba Mjini.*




*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mbeya, Bw. Lusekelo Joel Kajela, akielimisha wananchi kuhusu matumizi sahihi ya gesi ya kupikia (LPG), walipotembelea banda la Baraza wakati wa Bonanza la Nishati Safi ya Kupikia na Usafi wa Mazingira, lililofanyika katika viwanja vya Mwalambunge, Kata ya Lyela, Mbeya Mjini.*

ewura CCC
Consumer Consultative Council

# Waahidi kuwa mabalozi

Na Catherine Charles, Ilala

Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ilala Kasulu, iliyopo mkoani Dar es Salaam wameahidi kuwa mabalozi wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kwa lengo la kuielimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji, ili kupunguza gharama zisizo za lazima.

Ahadi hiyo waliitoa hivi karibuni, wakati wa utekelezaji wa programu ya uelimishaji iliyoandaliwa na Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji kwa Mkoa wa Kikazi wa Ilala, programu iliyowafikia wanafunzi 908 na walimu 34 wa shule hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya shule hiyo, Kaimu Mkuu wa Shule hiyo, Bw. George Mwanyama, alisema elimu waliyoipata kutoka EWURA CCC itawasaidia wanafunzi kuwa na matumizi sahihi na endelevu, hapo shuleni na wakiwa mabalozi kwa familia zao.

"Vijana hawa watakuwa mabalozi wazuri wa kuhamasisha jamii kuwa na matumizi sahihi ikiwemo kutunza miundombinu ya umeme na maji. Tunaishukuru sana EWURA CCC kwa kutuletea elimu hii muhimu," alisema Mwalimu Mwanyama.

Aidha, aliongeza kuwa walimu pia wamenufaika na elimu hiyo, hasa katika masuala ya utaratibu wa kuwasilisha malalamiko endapo watabaini changamoto au malalamiko kuhusu viwango vya ubora wa zinazotolewa.

"Tumefahamu mambo mengi ambayo hatukuyajua kabla. Sasa tupo tayari kutumia elimu hii katika maisha yetu ya kila siku," alisisitiza Mwanyama.

Kwa upande wake, Bi. Mary Nyato, ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji kwa Mkoa wa Kikazi wa Ilala, alisema Kamati imejipanga kuendelea kuwafikia wanafunzi na walimu wa shule mbalimbali katika mkoa huo ili kuwapatia elimu inayohusu haki na wajibu wao katika kupata huduma bora zinazodhibitiwa na EWURA.

"Ni muhimu kila mtumiaji wa huduma hizi kujua kwamba mtoa huduma ana viwango vya ubora anavyopaswa kufikia. Endapo viwango hivyo havifikiwi, ni wajibu wako mtumiaji kuwasilisha malalamiko yako," alisema Bi. Nyato.

Kamati hiyo imedhamiria kuendelea na kampeni ya utoaji elimu kwa makundi mbalimbali ya watumiaji wa huduma za nishati na maji, zikiwemo shule za sekondari na vyuo katika Mkoa wa Ilala, lengo likiwa ni kuhakikisha watumiaji wanapata elimu sahihi na uwezo wa kudai huduma bora na endelevu.



*Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC Ilala Bi. Catherine Charles (Katikati, waliosimama), akiwaelimisha wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ilala-Kasulu kuhusu huduma zinazodhibitiwa na EWURA wakati wa programu ya uelimishaji.*




*Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (BAWASA), Mhandisi Idd Yazid Msuya (Katikati), akiwa na Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Manyara, walipotembelea na kukagua maendeleo ya Mradi wa Maji wa Darda–Singu. Mradi huo unatarajiwa kuboresha huduma ya maji kwa zaidi ya wakazi 80,000 wa Wilaya ya Babati.*

# Huduma bora ya maji yaibua furaha Babati, Baraza latoa kauli

**Na Neema Nnko, Manyara**

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limeeleza kuridhishwa na utekelezaji mzuri wa mradi mkubwa wa maji safi yasiyo na chumvi katika Manispaa ya Babati, mkoani Manyara. Mradi huo umepunguza kwa kiasi kikubwa adha ya muda mrefu ya wakazi kupata maji yenye chumvi na magadi, hali iliyokuwa ikiathiri afya na maisha ya kila siku ya wananchi.

Akizungumza kwa niaba ya Baraza, Mjumbe wa EWURA CCC Mkoa wa Manyara, Bw. Deogratius Gallus, alisema kuwa mradi huo ni mfano bora wa mafanikio yanayopatikana kupitia ushirikiano kati ya wananchi, Serikali, watoa huduma, na wadau wa maendeleo.

"Baraza limekuwa mstari wa mbele katika kupokea na kufuatilia malalamiko ya watumiaji wa huduma ya maji, na kabla ya mradi huu, changamoto za maji yenye chumvi Babati zilikuwa zikitawala malalamiko hayo. Sasa tunaona matokeo chanya ya jitihada hizo," alieleza Bw. Gallus.

Mradi huo, unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (BAWASA), umefikia zaidi ya asilimia 98 ya utekelezaji na unatarajiwa kubadilisha kwa kiwango kikubwa maisha ya wakazi wa kata tatu za Bagara, Maisaka, na Babati Mjini.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa BAWASA, Mhandisi Iddi Msuya, mradi huo umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 12 na umehusisha ujenzi wa mtambo wa kuchakata maji pamoja na mtandao wa mabomba wenye urefu wa kilomita 78. Hadi sasa, zaidi ya wakazi 80,000 wameunganishwa na kupata huduma ya maji safi, yasiyo na chumvi.

Mhandisi Msuya alibainisha kuwa mafanikio ya mradi huu si tu kupatikana kwa maji salama bali pia kuchangia katika kuboresha afya, usafi na hali ya maisha ya wakazi wa Babati. Aidha, alitoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanatunza miundombinu ya mradi huo na kutumia maji kwa uangalifu ili mradi huo uwe endelevu kwa vizazi vijavyo.

Bi. Jasmin Ismaila, mkazi wa Bagara, ni miongoni mwa wananchi waliopokea kwa furaha kukamilika kwa mradi huo. Alieleza kuwa maji yenye chumvi yalikuwa yakiharibu nguo, vyombo na hata kuathiri ladha ya chakula.

"Kwa kweli huu ni mkombozi mkubwa kwetu. Tunashukuru kuona Serikali imetujali na kutupatia maji bora," alisema kwa furaha.

Mradi huu ulizinduliwa rasmi tarehe 16 Juni 2022 kwa uwekaji wa jiwe la msingi na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Sahil Geraruma. Huu ni mfano wa miradi inayojibu mahitaji halisi ya wananchi, kwa kutumia nguvu ya ushirikiano wa sekta mbalimbali, na inayowezesha utekelezaji wa haki ya msingi ya kupata maji safi na salama kwa kila Mtanzania.

# Ntendo wapata elimu juu ya matumizi sahihi ya nishati safi ya kupikia

Na Ramadhana Kakende, Rukwa

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) mkoani Rukwa limewapatia elimu wakazi wa Kijiji cha Fyengeleza, Kata ya Ntendo, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, kuhusu matumizi sahihi na salama ya nishati safi ya kupikia, hususan gesi za kupikia (LPG).

Elimu hiyo imetolewa kufuatia ombi la wananchi wa kijiji hicho baada ya kupokea mitungi ya gesi yenye ruzuku kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kama sehemu ya kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia majumbani.

Awali, baadhi ya wanakijiji walikuwa na hofu kubwa ya kutumia gesi, wakiihusisha na milipuko na hatari zingine za kiafya. Serikali ya kijiji, kupitia Afisa Mtendaji wake, Ndugu Basil Stima, iliwasiliana na EWURA CCC kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi hao ili kuwatoa hofu na kuwawezesha kutumia nishati hiyo kwa usalama.

Akizungumza wakati wa utoaji wa elimu hiyo, Bi Faustina Vallery, Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoa wa Rukwa, alisema gesi ni nishati safi, salama, na rafiki wa mazingira ambayo ikitumika kwa uangalifu huokoa muda, fedha na husaidia kuboresha afya za watumiaji.

"Wakazi wa Fyengeleza, nawaomba msiogope kutumia gesi kwani kuna faida nyingi, zikiwemo kupika haraka, kupunguza moshi unaodhuru afya, kutunza mazingira kwa kupunguza ukataji miti, na kuokoa muda na gharama kwa watumiaji nyumbani," alisema Bi Vallery.

Pia, alisisitiza kuwa mtungi wa gesi unapaswa kuhifadhiwa mbali na joto kali na kwamba hairuhusiwi kutumia vifaa vya moto kama vile simu ndani ya eneo la kupikia linalotumia gesi.

Baadhi ya wananchi walioshiriki semina hiyo walieleza kufurahishwa na elimu waliyoipata.

Ndugu Christopher Tung'ombe, mmoja wa wananchi hao alisema, "Nawashukuru sana EWURA CCC. Mmetutoa hofu na sasa tuko tayari kutumia gesi. Nitakuwa balozi kwa familia na marafiki kuhusu matumizi ya nishati hii safi ya kupikia na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa."

Naye Ndugu Idd Buda aliongeza kuwa tangu aanze kutumia gesi ameona mabadiliko makubwa katika matumizi ya muda, gharama na usafi wa mazingira.

"Gesi ni nafuu, salama na ya haraka. Ni suluhisho la muda mrefu kwa familia zetu, hivyo nawahamasisha wenzangu kuitumia kikamilifu."

Kwa upande wake Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Fyengeleza, Ndugu Basil Stima alimpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi, na pia alitoa pongezi kwa EWURA CCC kwa kutoa elimu ya matumizi sahihi na faida za nishati hii.

"Tunamshukuru Mheshimiwa Rais Samia kwa kuhimiza matumizi ya nishati safi, na pia tunalipongeza Baraza kwa kutufikia na kutuelimisha kuhusu matumizi sahihi na faida zake," alisema Bw. Stima.

Kampeni ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ni sehemu ya ajenda ya kitaifa ya kulinda mazingira na afya ya jamii. Kwa mkoa wa Rukwa pekee, serikali imetenga mitungi 9,750 ya gesi yenye ruzuku, ambayo itasambazwa katika wilaya zote tatu za mkoa huo.



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Rukwa, ndugu Dani Hinjo, akielekeza watumiaji wa Kijiji cha Fyengeleza, Kata ya Ntendo namna ya kutumia jiko la gesi, Manispaa ya Sumbawanga, hivi karibuni*



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Tabora, ndugu Willa Baraka Willa, akielimisha wanafunzi wa Shule ya Msingi Gongoni kuhusu kazi na majukumu ya Baraza.*

# 'Hatujui kusoma dira za maji': Tabora

**Na Sakina Yusuf, Tabora**

Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoa wa Tabora wamethibitisha kupokea maombi ya wananchi ya kutaka kupewa elimu juu ya namna ya kusoma mita za maji, na kuahidi kuyawasilisha kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora (TUWASA) ili hatua stahiki zichukuliwe haraka.

"Tumezisikiliza hoja zenu na tutafikisha maombi haya kwa TUWASA. Lengo ni kuhakikisha kila mtumiaji anaelewa matumizi yake na kuthamini bili anazopokea," alisema Bw. Abdul Mruma, Mjumbe wa Kamati hiyo, wakati wa programu ya uelimishaji iliyoandaliwa na EWURA CCC mwishoni mwa Machi 2025.

Maombi hayo yaliwasilishwa na wananchi wa Kata ya N'gambo, Manispaa ya Tabora, wakati wa mkutano wa hadhara kuhusu matumizi endelevu ya huduma za nishati na maji. Wananchi hao walieleza kuwa changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni kutokujua kusoma mita, jambo linalowafanya waishi kwa mashaka kuhusu uhalali wa bili wanazopokea kila mwezi.

Bi. Elizabeth Andrea, mkazi wa Mtaa wa Rwanzali, alisema "Sijui kusoma mita vizuri, hivyo siwezi kuthibitisha kama bili zetu zinaendana na matumizi halisi. Tunapokea mara nyingi bili kubwa, na hatujui kama kuna kasoro au matumizi yetu ni makubwa."

Mwenyekiti wa Mtaa wa Tukutuku, Bw. Emmanuel Kayamba, alieleza kuwa utoaji wa elimu hiyo utakuwa msaada mkubwa kwa wananchi katika kudhibiti matumizi yao, kuongeza uwazi, na kupunguza migogoro kati yao na mamlaka za maji.

> "
> **Wananchi wengi hawajui kusoma mita, na hii inawafanya wasidhibiti matumizi yao vizuri. Mafunzo yatasaidia kuondoa kutoaminiana**

"Wananchi wengi hawajui kusoma mita, na hii inawafanya wasidhibiti matumizi yao vizuri. Mafunzo yatasaidia kuondoa kutoaminiana," alisema.

Aliongeza kuwa ingawa TUWASA imekuwa ikitoa elimu kupitia vipeperushi na mitandao ya kijamii, njia hizo hazijawafikia wananchi wote ipasavyo, hivyo kuna haja ya kutumia mbinu za moja kwa moja kama mafunzo ya vikundi na mikutano ya ana kwa ana.

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), kupitia Kamati yake ya Mkoa wa Tabora, limesisitiza kuwa litaendelea kushirikiana na mamlaka husika kuhakikisha wananchi wanapata elimu muhimu kuhusu matumizi ya huduma wanazolipia. Baraza pia linaendelea kutumia majukwaa ya redio, mitandao ya kijamii, vipeperushi, na mikutano ya hadhara kufikisha elimu hiyo kwa jamii.

Kupitia juhudi hizi, Baraza linatarajia kuongeza uwazi katika utoaji wa huduma, kuimarisha uaminifu kati ya wananchi na watoa huduma, na kuchochea matumizi bora na ya uwajibikaji wa rasilimali ya maji kwa maendeleo endelevu ya jamii.



*Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC, Geita ndugu Wadi Omari akielimishaji kuhusu matumizi sahihi ya huduma za nishati na maji kwa wanafunzi wa moja ya Shule za Msingi mkoani humo hivi karibuni.*

# EWURA CCC yajibu sauti ya mwanafunzi, yatatua kero ya nguzo ya umeme Geita

**Na Wadi Omary, Geita**

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limeonesha kwa vitendo dhamira yake ya kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati, baada ya kuongoza jitihada zilizowezesha kuondolewa kwa nguzo ya umeme iliyokuwa katikati ya uwanja wa michezo wa Shule ya Msingi Uwanja, Manispaa ya Geita.

Tukio hilo lilikuja baada ya mwanafunzi wa shule hiyo, Rajabu Juma, kubainisha changamoto hiyo wakati Baraza likitoa elimu kuhusu haki na wajibu wa watumiaji wa huduma za nishati na maji. Nguzo hiyo ilikuwa imekuwa kikwazo kikubwa kwa matumizi salama ya uwanja huo na kuhatarisha maisha ya wanafunzi.

Akizungumza kwa niaba ya shule, Mwalimu Mkuu Selemani Mabeyo alithibitisha kuwa tatizo hilo lilidumu kwa muda mrefu licha ya juhudi zilizofanywa kuwasiliana na TANESCO na mamlaka nyingine husika. “Tumekuwa tukiwasiliana mara kwa mara na TANESCO pamoja na Halmashauri, lakini hatukufanikiwa,” alisema Mwalimu Mabeyo.

> **“Tunalifahamu tatizo hili, na tumepanga kuiondoa nguzo hiyo ndani ya siku tatu... Tunawashukuru sana EWURA CCC kwa kutusikiliza na kuhakikisha nguzo imeondolewa. Sasa wanafunzi wetu watafurahia michezo bila hofu**

Baada ya EWURA CCC kupokea malalamiko hayo, ilichukua hatua za haraka kuwasiliana na Meneja wa TANESCO mkoa wa Geita, Mhandisi Joachem Ruweta, ambaye alikiri kuwepo kwa tatizo hilo na kueleza kuwa lilitokana na maandalizi ya ujio wa Mwenge wa Uhuru mwaka 2024 ambapo uwanja huo ulipangwa kutumika kwa shughuli hiyo.

“Tunalifahamu tatizo hili, na tumepanga kuiondoa nguzo hiyo ndani ya siku tatu,” alisema Mhandisi Ruweta. Ahadi hiyo ilitekelezwa kwa haraka na hatimaye nguzo hiyo iliondolewa, na uwanja huo sasa unatumika kwa usalama bila kikwazo.

Hatua hiyo ilipokelewa kwa furaha na wanafunzi pamoja na walimu wa shule hiyo. “Tunawashukuru sana EWURA CCC kwa kutusikiliza na kuhakikisha nguzo imeondolewa. Sasa wanafunzi wetu watafurahia michezo bila hofu,” alisema Mwalimu Mabeyo.

Tukio hili linathibitisha nafasi ya EWURA CCC kama kiunganishi muhimu kati ya watoa huduma na wananchi, sambamba na kuendeleza jitihada za kuhakikisha huduma za nishati zinatolewa kwa usalama, ufanisi na kuzingatia maslahi ya watumiaji.

# Hamasisheni uvunaji wa maji ya mvua: Ngula

Na Geofrey Sokesia, Singida

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limeshauri Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA) kuhamasisha wakazi wa Manispaa ya Singida kuvuna na kutumia maji ya mvua ili kusaidia kupunguza changamoto ya uhaba wa maji katika mji huo.

Ushauri huo umetolewa na Wajumbe wa EWURA CCC walipotembelea ofisi za SUWASA kwa madhumuni ya kufahamu hali ya utoaji wa huduma, changamoto zinazokabili Mamlaka hiyo, na kujadili hatua madhubuti za kuboresha huduma kwa watumiaji.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Mwenyekiti wa Baraza, Mhandisi David Ngula, alisema kuwa kuvuna maji ya mvua ni hatua mbadala na muhimu katika kipindi ambacho SUWASA inazalisha lita milioni 10.5 za maji kwa siku dhidi ya mahitaji ya zaidi ya lita milioni 23.3 kwa siku.

"Wananchi wakihamasishwa kujenga makaro au matanki ya kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya nyumbani, itasaidia kupunguza utegemezi kwa huduma ya bomba, hasa kipindi cha kiangazi," alisema Mhandisi Ngula, akisisitiza umuhimu wa kutoa elimu kuhusu ujenzi wa visima vya kuvunia maji kwa usalama.

Akitoa mrejesho kwa niaba ya SUWASA, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Bw. Sebastiani Warioba, alisema Mamlaka yake, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Singida tayari imeanza kuchukua hatua za kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua, ikiwa ni pamoja na kutaka michoro ya nyumba mpya kuonesha eneo la kuvunia maji.

"Ramani za nyumba zinazowasilishwa kwa ajili ya kupata vibali vya ujenzi sasa zinatakiwa kuonesha eneo la karo au tanki la kuvunia maji ya mvua. Tunashirikiana na halmashauri kulisimamia hili kwa karibu," alisema Warioba.

Mbali na juhudi hizo, SUWASA inatekeleza Mradi wa Miji 28 kwa ajili ya kuchimba visima vipya 12 na kufufua visima vilivyokuwa havitumiki, sambamba na kudhibiti upotevu wa maji kwa kubadilisha mabomba chakavu na kuziba mivujo kwa haraka.

Katika hatua za kukabiliana na wizi wa maji, Warioba alieleza kuwa SUWASA imeanzisha mfumo wa zawadi kwa wananchi wanaotoa taarifa sahihi kuhusu wizi huo, huku ikiahidi kutunza usiri wa watoa taarifa ili kuongeza ushirikiano kutoka kwa jamii.

Wakati wa ziara hiyo, Wajumbe wa Baraza walitembelea chanzo cha maji cha Irao, eneo la uchimbaji wa kisima kipya katika Kata ya Mwankoko, na mradi wa ujenzi wa bwawa la majitaka eneo la Manga, ili kupata uelewa wa kina kuhusu hali ya huduma za maji na kupanga mikakati ya utetezi wa maslahi ya watumiaji kwa ufanisi zaidi.

Kupitia ziara hizo na mashauriano yanayoendelea, EWURA CCC inaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya maji nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora, salama na endelevu, sambamba na kuelimishwa kuhusu haki na wajibu wao kama watumiaji wa huduma hizo muhimu.



*Meneja Uzalishaji Maji na Usambazaji Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (wa pili kushoto) ndugu Elisha Kivuyo, akitoa maelezo kwa Ujumbe wa Baraza ulipoitembelea mamlaka hiyo hivi karibuni.*

# HabariPicha



*Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC, Rukwa ndugu Ramadhan Kakende akionesha kwa vitendo matumizi ya jiko la gesi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kwenye viwanja vya Mandela, Manispaa ya Sumbawaga.*



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Rukwa, Bi. Leah Sanga, akionesha kwa vitendo matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kutumia gesi kwa wananchi wa kijiji cha Fyengeleza, Kata ya Ntendo, Manispaa ya Sumbawanga.*



*Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Lindi Bi. Fatuma Nyama akielimisha wanachama wa vikundi vya Wanawake wanaolima zao la Mwani eneo la Mchinga II, Manispaa ya Lindi.*



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Shinyanga (kulia) ndugu Joseph Ndatala, akiongea na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga, Mhandisi Yusuph Katopola alipotembelea Mamlaka hiyo hivi karibuni.*



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Mtwara ndugu Said Ismail, akielimisha wananchi kuhusu haki na wajibu wao pamoja na utaratibu wa kuwasilisha malalamiko kupitia EWURA CCC, katika shughuli ya Maulid iliyofanyika Kata ya Mitengo, Manispaa ya Mtwara.*



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Simiyu ndugu Bahati Patrick, akiwaelimisha wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mwabasabi mjini Simiyu kuhusu majukumu ya Baraza.*

ewura CCC
Consumer Consultative Council

# Kongole EWURA CCC kwa elimu kupitia redio



*Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC Geita, ndugu Wadi Omari, akitoa elimu kwa jamii kupitia redio Storm FM iliyopo mjini Geita.*

**Na Wadi Omari, Geita**

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limepokea pongezi kutoka kwa wananchi wa mkoa wa Geita kwa kutoa elimu ya haki, wajibu na utumiaji bora wa huduma za nishati na maji kupitia kipindi cha redio kinachorushwa kila Jumatano jioni kupitia Storm FM Radio.

Mathias Ruben, mkazi wa Mtaa wa Nyankumbu, alieleza jinsi elimu hiyo ilivyowasaidia kupata huduma bora za maji kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita (GEUWASA).

"Licha ya matatizo ya muda mrefu ya upatikanaji wa maji, elimu ya EWURA CCC kupitia vipindi vya redio ilituwezesha kupata uelewa wa namna sahihi ya kuwasilisha malalamiko yetu na hatimaye kupata huduma," alisema Ruben.

Alieleza kuwa, baada kupata elimu kupitia redio hiyo, walibaini kuwa utaratibu sahihi wa kutatua malalamiko yao ya maji ni kwa kuyawasilisha GEUWASA kwa njia ya maandishi na kuipa nakala EWURA CCC nakala ya lalamiko hilo kwa ajili ya ufuatiliaji.

"Kupitia elimu tuliyopata redioni, tulielewa kuwa njia sahihi ya kuwasilisha malalamiko yetu ya huduma ya maji ni kwa maandishi kwenda GEUWASA, huku tukitoa nakala EWURA CCC kwa ajili ya ufuatiliaji," alisema Ruben.

Naye Katibu wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Geita, Bw. Khalphan Msemo, aliwahakikishia wananchi kuwa EWURA CCC itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha jamii kwa njia za kisasa ili kuhakikisha watumiaji wanajua haki na wajibu wao.

"Kupitia vipindi vya redio na majukwaa mbalimbali, tunalenga kuwajengea wananchi uwezo wa kudai huduma bora na kushiriki kikamilifu katika utetezi wa haki zao," alisema Khalphan.

Aliongeza kuwa pongezi hizi zinadhihirisha kuwa juhudi za Baraza zinapata mwitikio mzuri katika jamii na zinaendelea kuwa daraja la karibu kati ya watumiaji na watoa huduma kwa kuleta taarifa sahihi, utatuzi wa kero, na uhamasishaji wa umma.



# TGDC yapongezwa Mradi wa Umeme wa Jotoardhi

Na Mwasiti A. Majengo, Mbeya

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limepongeza hatua muhimu zilizofikiwa na Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania (TGDC) katika utekelezaji wa mradi wa kimkakati wa uzalishaji wa umeme kwa njia ya jotoardhi unaotekelezwa katika eneo la Ngozi, Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya.

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa Baraza hilo, Mhandisi David Ngula, wakati wa ziara ya kitaalamu ya Wajumbe wa EWURA CCC waliotembelea eneo hilo kwa lengo la kujionea hali halisi ya maendeleo ya mradi na kujiridhisha na namna utekelezaji wake unavyozingatia maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati nchini.

Mhandisi Ngula alieleza kuwa, Mradi wa Jotoardhi unaotekelezwa na TGDC ni wa kipekee na unatoa matumaini makubwa kwa nchi katika kufikia malengo ya kuwa na vyanzo vya nishati mbadala, endelevu na rafiki kwa mazingira.

Alisema kuwa Mradi huo unaendana kikamilifu na ajenda ya serikali ya kuwa na nishati ya uhakika, inayopatikana kwa gharama nafuu na isiyoathiri mazingira kwa kiasi kikubwa.

"Mradi huu si tu kwamba utaongeza uwezo wa taifa kuzalisha umeme, bali pia unatoa fursa za ajira, ujuzi mpya wa teknolojia, na kuinua uchumi wa maeneo yanayozunguka mradi. Kama Baraza, tupo hapa kuona kama watumiaji wananufaika, wanashirikishwa na wanaelewa mradi huu unamaanisha nini kwao," alisema Mhandisi Ngula.

Akitoa maelezo ya kitaalamu kuhusu Mradi huo, Mhandisi Juma Mlingwa kutoka TGDC ilibainika kuwa, Mradi huo unalenga kuzalisha megawati 70 za umeme kupitia visima vitatu vikuu vya jotoardhi, yaani NB-1, NB-5, na NZB-3 na kwamba kwa sasa kazi ya uchimbaji inaendelea kwenye kisima cha NZB ambacho peke yake kinatarajiwa kuzalisha hadi megawati 30, kiwango kinachoweza kusaidia kuhudumia zaidi ya kaya 100,000.

> "Nishati ya jotoardhi inaweza kutumika zaidi ya uzalishaji wa umeme, ikiwemo kuendeleza shughuli za kilimo kama kukausha mazao, kutotolesha vifaranga, na matumizi ya viwandani

Alifafanua kuwa "Tofauti na vyanzo vingine vya nishati, jotoardhi haitegemei misimu ya mvua au jua, jambo linaloifanya kuwa chanzo cha uhakika kwa muda mrefu na kuongeza kuwa, teknolojia ya jotoardhi haichafui mazingira na inaendana na malengo ya kitaifa ya kuhifadhi mazingira na kupunguza hewa ukaa.

Mwanajiolojia Mwandamizi kutoka TGDC, Ndugu Lucas Tumbu, naye alieleza kuwa, "Nishati ya jotoardhi inaweza kutumika zaidi ya uzalishaji wa umeme, ikiwemo kuendeleza shughuli za kilimo kama kukausha mazao, kutotolesha vifaranga, na matumizi ya viwandani."

Alisema TGDC inalenga kuzalisha jumla ya megawati 200 kutoka maeneo mbalimbali ya jotoardhi nchini ifikapo mwisho wa mwaka 2025.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mkoa wa Mbeya (Mbeya RCC), Bw. Philemon Mwansasu alisisitiza kuwa uwekezaji wa TGDC ni wa mfano, na ni ushahidi kuwa Tanzania inaweza kutumia maarifa ya kisasa kuongeza tija katika sekta ya nishati.

Ziara hiyo ya Baraza si tu ililenga kufuatilia maendeleo ya mradi, bali pia ni sehemu ya jukumu lake la msingi la kulinda na kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za nishati na maji.

Kwa kutembelea miradi mikubwa kama ya jotoardhi, Baraza linajihakikishia kuwa mtumiaji wa mwisho wa huduma si mtazamaji tu, bali ni mshiriki mwenye haki, anayestahili sauti na faida katika mnyororo mzima wa nishati nchini.




*Mhandisi Mlingwa Juma kutoka TGDC akifafanua kuhusu Mradi wa Uzalishaji Umeme kwa njia ya Jotoardhi katika eneo la Ngozi, Wilayani Rungwe, mkoa wa Mbeya.*




*Vifaa vya kupikia vinavyotumia nishati safi ya umeme havina moshi hatari kwa afya yako, hulinda mazingira na kuokoa muda.*

# Mkakati mpya unavyoboresha afya na mazingira yako

**Na Sakina Yusuf, Tabora**

Hebu fikiria jioni tulivu ukiwa nyumbani kwako na mara harufu nzuri ya chakula inasambaa, lakini hauoni moshi unaokukera machoni au kukufanya ukohoe! Huku ndiko kupika kwa kutumia nishati safi ya kupikia.

Kupika ni jambo lisiloepukika katika familia, kama ilivyo kwenye taasisi, au mikutano inayohitaji watu kupata huduma ya chakula. Hata hivyo, nishati zisizofaa zinazotumika kupika chakula zinaweza kuwa na athari kubwa kwa afya za watumiaji na kwa mazingira.

Katika kudhibiti athari za kimazingira na kiafya zitokanazo na nishati za kupikia zisizo salama kama vile kuni na mkaa, Serikali ya Tanzania imeandaa na kuanza kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2024-2034, lengo likiwa kuhakikisha kuwa kufikia mwaka 2034 asilimia 80 ya watanzania wote wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

Mkakati huu ni ufunguo wa kila mtanzania, kulinda afya yake, jamii, na kutunza mazingira kwa maisha endelevu. Na sasa hebu tuzitazame faida chache za Mkakati huu, hususani faida za kupika kwa kutumia nishati safi.

> **"Katika kudhibiti athari za kimazingira na kiafya zitokanazo na nishati za kupikia zisizo salama kama vile kuni na mkaa, Serikali imeandaa na kuanza kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2024-2034**

**Faida za kutumia nishati safi ya kupikia ni pamoja na:**

i. Kutunza afya yako na ya familia: Jiko lako linapaswa kuwa chanzo cha chakula, si cha magonjwa. Moshi unaotokana na kuni na mkaa umejaa sumu ambazo ni hatari kwa afya hasa za wanawake na watoto kwani wao ndio hushughulika zaidi na masuala ya jikoni. Ukiwa na jiko linalotumia nishati safi litakukinga na haya yote na hivyo utakuwa unafanya uwekezaji kwenye uhai wako na familia yako.

ii. Kuokoa muda: Fikiria muda unaopotea kila siku kwenda kutafuta kuni au kusubiri mkaa uwe tayari. Majiko ya umeme, gesi, au sola ni kama maajabu jikoni kwako. Haya yanakuwezesha kuwasha kwa urahisi, kupika haraka, na kukuacha na muda wa ziada kufanya shughuli zingine za kiuchumia na kijamii. Muda uliookolewa ni zawadi isiyo na bei.

iii. Nishati safi huokoa fedha: Mwanzoni, kununua jiko safi inaweza kuonekana kama gharama kubwa hata hivyo baadae utashangaa ni kiasi gani unaokoa fedha zako kwani umeme na gesi, zikitumiwa vizuri zitaokoa fedha zako.

Kulingana na tafiti zilizofanywa na Chama cha Nishati Jadidifu Tanzania (TAREA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), nishati ya

> Mbali na manufaa yanayokuja kwa kutumia nishati safi ya kupikia, bado kuna changamoto zinazoweza kusababisha kuchelewa kufikia lengo la asilimia 80 ya watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2034 kama inavyobainishwa na Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2024-2034.

> Mbinu nyingine ni kuhamasisha wananchi na taasisi kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kutumia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na kutoa elimu kwa wananchi kupitia mikutano, warsha na mikusanyiko ya wananchi ili wananchi wapate kuelewa umuhimu wa matumizi ya nishati safi.

umeme hasa ikitumika kwa majiko yenye ufanisi "Induction" au sufuria za presha za umeme "Electric Pressure Cookers – EPCs" inaweza kuwa nafuu zaidi. Kwa mfano:-

• Kupika maharage nusu kilo:

Umeme (kwa kutumia EPC): Utatumia takriban Shilingi 180 tu.

Mkaa: Utatumia takriban Shilingi 1,180

Gesi (LPG): Utatumia takriban Shilingi 800.

Mafuta ya taa: Utatumia takriban Shilingi 600.

Hii inaonesha kuwa kwa mfano wa kupika maharage, kwa presha ya umeme inaweza kuwa nafuu mara 5 hadi 6 kuliko gesi, na karibu mara 6 kuliko mafuta ya taa, na zaidi ya mara 5 kuliko mkaa.

Hii ni kwa mujibu wa makala iliyoandikwa na Herieth Makweta katika tovuti ya Mwananchi tarehe 13 Machi 2024 "Kupikia umeme ni nafuu kuliko nishati nyingine." https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/kupikia-umeme-ni-nafuu-kuliko-nishati-nyingine-tafiti-4555400

iv. Kutunza mazingira: Kutumia nishati safi ya kupikia husaidia kutunza mazingira kwa kupunguza ukataji wa miti unaotokana na matumizi ya kuni na mkaa. Hii hupunguza uharibifu wa misitu, mmomonyoko wa udongo, na kuchangia kupungua kwa hewa ukaa (carbon emissions) inayochochea mabadiliko ya tabianchi. Kwa kutumia nishati safi, jamii hushiriki moja kwa moja katika kulinda mazingira na kuhakikisha rasilimali za asili zinadumu kwa vizazi vijavyo.

Mbali na manufaa yanayokuja kwa kutumia nishati safi ya kupikia, bado kuna changamoto zinazoweza kusababisha kuchelewa kufikia lengo la asilimia 80 ya watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2034 kama inavyobainishwa na Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia 2024-2034. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:

1. Uelewa mdogo wa wananchi na taasisi kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia,

2. Uhaba wa malighafi na miundombinu ya upatikanaji wa nishati safi ya kupikia nchini,

3. Gharama kubwa ya awali na matumizi ya nishati safi, kama vile vifaa na majiko sanifu ya kupikia, na

4. Uwekezaji mdogo katika nishati safi ya kupikia.

Katika kuhakikisha changamoto hizi zinatatuliwa, Serikali katika Mkakati huo, imeeleza mikakati itakayotumika katika kutatua changamoto hizi zikiwa ni pamoja na kuongeza uelewa wa wananchi na taasisi kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mkakati huo unaonesha kuwa serikali itaongeza uelewa kwa umma kwa kutoa elimu kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na athari za kiafya na kimazingira zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia.

Mbinu nyingine ni kuhamasisha wananchi na taasisi kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kutumia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na kutoa elimu kwa wananchi kupitia mikutano, warsha na mikusanyiko ya wananchi ili wananchi wapate kuelewa umuhimu wa matumizi ya nishati safi.

Baraza linaunga mkono kikamilifu mkakati huu kwa kuendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kutumia nishati safi kwa ajili ya kupikia. Kupitia kampeni zake za uhamasishaji katika mikutano ya hadhara, maonesho ya kitaifa, warsha, klabu za wanafunzi, na vyombo vya habari, EWURA CCC imekuwa ikiwafikia wananchi moja kwa moja na kutoa elimu kuhusu faida za kiafya, kiuchumi na kimazingira za kutumia nishati safi kama gesi, umeme au biogas badala ya kuni na mkaa. Baraza pia huwahimiza wananchi kuchukua hatua madhubuti za kulinda afya zao na mazingira kwa kuachana na nishati chafu.

Aidha, Baraza hutumia majukwaa ya mitandao ya kijamii, vipindi vya redio na televisheni, pamoja na ushirikiano na mamlaka nyingine serikalini kueneza ujumbe wa matumizi ya nishati safi kwa umma. Kwa kufanya hivyo, Baraza linachangia moja kwa moja utekelezaji wa mkakati huo kwa kuongeza uelewa wa wananchi na kushirikiana na serikali kuhamasisha mabadiliko ya tabia katika jamii.

# Watakiwa kutoa elimu kuhakikisha usalama wa watumiaji

Na Evarista Lucas, Singida

Wakati taifa likihamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imetoa wito kwa wauzaji na wasambazaji wa mitungi ya gesi mkoani Singida kuhakikisha wanatoa elimu ya kutosha kwa watumiaji kuhusu matumizi sahihi na tahadhari za usalama za bidhaa hiyo muhimu.

Wito huo umetolewa na Mhandisi wa Petroli kutoka EWURA, Bw. Mbarouk Shaame, wakati wa semina ya mafunzo kwa wauzaji na watumiaji wa gesi iliyoandaliwa na ofisi ya EWURA Kanda ya Kati. Semina hiyo ililenga kuimarisha uelewa kuhusu usalama wa matumizi ya gesi, sambamba na kuondoa hofu isiyo ya lazima inayowakumba baadhi ya watumiaji.

"Ni wajibu wa kila muuzaji wa gesi kuwapa wateja wake elimu sahihi na ya mara kwa mara kuhusu matumizi bora na salama ya gesi ya kupikia. Kukosekana kwa elimu hii kunaongeza uwezekano wa ajali kama vile mlipuko, moto au majeraha, hasa nyumbani ambako mitungi mingi hutumika," alisema Mhandisi Shaame.

Aliongeza kuwa baadhi ya wauzaji wamekuwa wakijikita katika biashara bila kuweka matangazo ya tahadhari au maelekezo ya usalama katika maeneo yao ya kuhifadhi mitungi (gas cages), hali inayoweka maisha ya wateja wao katika hatari.

Mhandisi Shaame alitoa mfano wa mitungi kubebwa kwa ulalo, namna ambayo isiyo salama, kushushwa ovyo bila kujua kama kuna uvujaji, au kutumika karibu na vyanzo vya moto bila tahadhari stahiki.

"Mtungi wa gesi haupaswi kubebwa ukiwa umelala au kuutumia moja kwa moja mara baada ya kununuliwa. Inashauriwa kusubiri walau kwa dakika 20 baada ya kuusafirisha ndipo uanze kuutumia. Pia mitungi haipaswi kuwekwa karibu na jiko la mkaa au moto unaowaka," alisisitiza Mha. Shaame.

Katika kuhakikisha matumizi ya gesi yanakuwa salama, alikumbusha pia kuwa ni wajibu wa wauzaji kuwa na mizani ya kupimia kiasi cha gesi kinachouzwa, kama ambavyo inatakiwa kisheria kwa mujibu wa taratibu za EWURA na sheria ya vipimo nchini.

Kwa upande wake, mmoja wa wasambazaji wa gesi mkoani Singida, Bw. Anael Kisamo ambaye pia alinufaika na semina hiyo, aliomba EWURA kusaidia kutoa elimu kwa wananchi kuondoa dhana potofu kuhusu mitungi iliyopauka rangi.

"Wateja wengi hukataa kuchukua mitungi ambayo rangi yake imefifia, wakiamini ni mibovu. Hali hii huleta changamoto kwani biashara ya gesi hufanyika kwa kubadilishana mitungi, ambapo mtu hapati mtungi alioleta bali mwingine uliopo sokoni," alisema Kisamo.

Kisamo alisema pamoja na wao kuwa na wajibu wa kuwapa elimu wateja juu ya matumizi na hatari zinazoweza jitokeza katika kutumia gesi, aliiomba EWURA na Baraza la Ushauri la watumiji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) kusaidia kuwapa elimu watumiaji wa gesi kuhusu mitungi ya gesi iliyofifia rangi kuwa haina madhara yoyote na hivyo waitumie pasipo na shaka yoyote.

Aidha, Bi. Salome Mkama, mmoja wa watumiaji wa gesi aliyepata fursa ya kushiriki semina hiyo, alisema elimu aliyoipata imemsaidia kujua matumizi salama ya gesi na ameahidi kuitoa kwa jamii yake.

"Naomba elimu hii iendelee kusambazwa kwa wananchi zaidi, lakini pia tuiombe serikali itusaidie kushusha bei ya gesi ili kila Mtanzania aweze kumudu gharama za kutumia nishati hii safi," alisema Mkama.

Kwa upande wake Bi. Theresia Mande, Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji mkoani Singida (RCC) ambaye pia alishiriki katika semina hiyo, aliwahimiza wauzaji wa gesi kuzingatia miongozo ya Serikali na kusikiliza maoni ya wateja wao.

"Katika kazi zetu za kutoa elimu kwa jamii, EWURA CCC imeendelea kuwahamasisha wananchi kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia. Gesi ni moja ya nishati bora, lakini jamii yetu inahitaji kupata maarifa sahihi ili kuitumia kwa usalama," alisema Bi. Mande.

Mafunzo haya na mijadala ya wadau yameonesha kuwa pamoja na changamoto zilizopo, kuna fursa kubwa ya kuifanya gesi ya kupikia kuwa chaguo la msingi kwa familia nyingi nchini. Hii ni iwapo elimu sahihi itatolewa, bei zinakuwa rafiki, na usambazaji utapanuliwa hadi maeneo ya vijijini.



# 'Maboresho ya mikataba yaweke msingi wa haki na wajibu wa watumiaji'



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Mbeya Bw. Lusekelo Kajela akizungumza wakati wa utoaji maoni kuhusu Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa Mbeya UWSA.*

**Na Mwasiti A. Majengo, Mbeya**

Katika kuimarisha uelewa wa watumiaji wa huduma za maji kuhusu haki na wajibu wao, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) Mkoa wa Mbeya limependekeza kuwekwa kwa kipengele mahsusi cha haki na wajibu wa mteja katika mkataba mpya wa huduma wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya UWSA).

Pendekezo hilo lilitolewa na Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma Mkoa wa Mbeya (Mbeya RCC), Bw. Lusekelo Kajela, katika kikao cha kukusanya maoni ya wadau kuhusu maboresho ya mkataba huo, kilichofanyika katika ukumbi wa Mbeya UWSA, Mtaa wa Sabasaba.

"Mkataba wa huduma haupaswi kuwa wa kiufundi pekee, bali uwe chombo cha maelewano ya kijamii, kisheria na kiutawala. Maelezo ya haki na wajibu yakiwa wazi katika mkataba, hujenga msingi wa uwajibikaji na huzuia migogoro isiyo ya lazima," alisisitiza Bw. Kajela.

Alibainisha kuwa baadhi ya changamoto zinazowakumba watumiaji wa huduma, kama vile kutolipwa fidia au kukatiwa huduma bila taarifa, hutokana na kukosekana kwa uelewa wa wajibu na haki zao, jambo ambalo linaweza kuzibwa kwa kuwepo kwa mkataba wenye vipengele vya kielimu kwa mlaji.

Katika kikao hicho, Kamati ya Watumiaji pia ilitumia fursa hiyo kutoa elimu kwa washiriki 241 waliokuwepo, kuhusu kazi za Baraza, njia sahihi za kuwasilisha malalamiko, na haki za msingi za watumiaji wa huduma kama vile haki ya kuelimishwa, kusikilizwa, na kupata huduma bora kwa wakati.

"Tunapojenga uwezo wa watumiaji wa huduma kwa kuwafahamisha haki na wajibu wao, tunaongeza pia uwajibikaji wa watoa huduma. Hili ni jukumu la msingi la Baraza," aliongeza Bw. Kajela.

Afisa Mahusiano wa Mbeya UWSA, Bi. Neema Stanton, alikiri kupokea kwa mikono miwili mapendekezo yaliyotolewa na EWURA CCC na wadau wengine, akibainisha kuwa mamlaka hiyo iko tayari kufanya maboresho yanayolenga kuwajengea wateja imani zaidi.

"Tunatambua na kuthamini mchango wa Baraza. Maoni na ushauri mliotoa si wa kupuuzwa, bali ni dira katika kuhakikisha tunaboresha mkataba huu kwa manufaa ya wote kwa maana ya Mamlaka na wananchi," alisema Bi. Stanton.

Mbeya UWSA iko katika hatua ya mwisho ya kukamilisha maboresho ya mkataba huo wa huduma kwa wateja, hatua ambayo inatarajiwa kuleta uboreshaji mkubwa wa uwazi na uwajibikaji kati ya mtoa huduma na mtumiaji.

ewura CCC
Consumer Consultative Council

# Kwa nini huduma rasmi za maji ni muhimu kwa maendeleo endelevu

Na Emmanuel Paul, Mtwara

Katika kila tone la maji kuna uhai, afya na maendeleo. Hata hivyo, si kila huduma ya maji ni salama, ya kuaminika, au endelevu. Serikali ya Tanzania imechukua hatua makini kwa kuanzisha mamlaka rasmi za usambazaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira ili kuhakikisha huduma bora kwa wananchi.

Makala hii inachambua kwa kina sababu za msingi zinazopaswa kuwahamasisha wananchi kutumia huduma za maji zinazodhibitiwa kisheria kwa ajili ya ustawi wa jamii na vizazi vijavyo.

**1. Ulinzi wa aaki kupitia mfumo wa kisheria**

Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414, inalinda haki ya mtumiaji wa huduma ya maji. Kifungu cha 34 ya sheria hiyo kinataja wazi kuwa EWURA ina mamlaka ya kushughulikia malalamiko yoyote kuhusu usambazaji au ubora wa huduma kutoka kwa mtoa huduma anayedhibitiwa.

Hii inaipa jamii msingi wa kisheria wa kudai huduma bora, zenye gharama stahiki, na zinazokidhi viwango vya afya. Wananchi wanaotumia huduma rasmi wanakuwa na nafasi ya kisheria ya kulinda haki zao.

**2. Utatuzi wa haraka wa malalamiko bila urasimu**

EWURA na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) wameweka mfumo rafiki na usio na urasimu wa kushughulikia malalamiko. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa kwa mtoa huduma au kupitia Baraza, ndani ya kipindi cha miezi 12 hadi 24 baada ya tatizo kujitokeza.

Mfumo huu unalenga kuhakikisha kuwa haki za watumiaji hazikandamizwa kwa sababu ya ukosefu wa uelewa au urasimu wa kiofisi.

**3. Uhakika wa maji salama kwa afya ya familia**

Mamlaka rasmi za maji huchukua hatua madhubuti kupima ubora wa maji kwa kufuata viwango vya kitaifa vya afya. Hii inalinda jamii dhidi ya magonjwa yanayosababishwa na maji machafu kama kipindupindu, typhoid, na minyoo.

Kwa kutumia huduma zisizodhibitiwa, familia hujiweka kwenye hatari ya kiafya na huongeza gharama za matibabu zisizokuwa za lazima.

**4. Uendelevu wa miundombinu kwa maendeleo ya Taifa**

Mamlaka za maji si tu watoa huduma, bali pia wasimamizi wa miundombinu ya maji. Hii ni pamoja na matangi, pampu, mabomba, na matengenezo ya kila siku. Mapato kutoka kwa wateja yanasaidia kuimarisha huduma, kupanua maeneo ya upatikanaji, na kuajiri wataalamu wa sekta.

Huduma zisizo rasmi mara nyingi hukosa uwezo huu wa uwekezaji na uendelevu.

**5. Ushirikiano na Serikali na Wadau wa Maendeleo**

Mamlaka rasmi hushirikiana kwa karibu na Serikali na mashirika ya kimataifa kutekeleza miradi mikubwa ya maji. Ushirikiano huu huwezesha uwekezaji mkubwa, uboreshaji wa teknolojia, na upatikanaji wa huduma kwa maeneo mengi zaidi ya nchi.

Wananchi wanaotumia huduma rasmi huwa sehemu ya mfumo wa kitaifa wa maendeleo, tofauti na watumiaji wa vyanzo visivyo rasmi ambavyo havishirikishwi katika mipango ya kitaifa.

**Hitimisho**

Matumizi ya huduma rasmi za maji ni njia salama na endelevu ya kulinda afya, kudai haki, na kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kupitia usimamizi wa EWURA, uelimishaji wa EWURA CCC, na ushirikiano wa wananchi, Tanzania inaweza kujenga mfumo wa maji unaoaminika, unaowajibika, na unaozingatia usawa wa huduma.

Huu si wajibu wa mamlaka pekee, bali ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha tunatumia huduma rasmi kwa manufaa yetu sote—leo na kwa vizazi vijavyo.









# Baraza lajikita katika maadili kuimarisha utetezi wa watumiaji

Na Chipegwa Samwel, Morogoro

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) limejipambanua kama chombo madhubuti cha kutetea haki za watumiaji kwa kuongozwa na nguzo tisa za maadili. Nguzo hizi zimekuwa dira na msingi wa utekelezaji wa kazi za Baraza kwa uadilifu, uwazi, na uwajibikaji kwa jamii.

Katibu Mtendaji wa EWURA CCC, Bi. Stella Lupimo, alieleza kuwa maadili hayo si maneno tu yaliyoandikwa, bali ni mwongozo hai unaotumika kila siku katika utendaji kazi, mawasiliano na maamuzi ya Baraza, Sekretarieti na Kamati za Watumiaji wa Huduma za Mikoa (RCCs).

"Nguzo hizi zimejenga utambulisho wetu kama chombo cha uwakilishi wa wananchi. Zinatusaidia kuimarisha uaminifu, ushirikiano na kuwajibika kwa kila hatua tunayochukua kwa niaba ya watumiaji," alieleza Bi. Lupimo.

Nguzo hizo tisa ni:

- Uadilifu (Integrity): Baraza linashikilia misingi ya ukweli, uaminifu na kupinga vitendo vya kifisadi. Kila maamuzi hufanyika kwa haki bila upendeleo.
- Uwajibikaji (Accountability): Baraza linawajibika kwa wananchi kwa kuhakikisha kuwa sauti zao zinasikika na changamoto zao zinashughulikiwa kikamilifu.
- Weledi (Professionalism): Wajumbe na watendaji wake hutekeleza majukumu kwa maarifa, ufanisi na kufuata viwango vya kitaaluma vilivyowekwa.
- Ushirikiano (Teamwork): Mafanikio ya Baraza yanajengwa kupitia ushirikiano thabiti na watoa huduma, mamlaka, na wananchi.
- Uwazi (Transparency): Baraza linahakikisha taarifa kuhusu kazi zake, changamoto na mafanikio zinapatikana kwa umma kwa urahisi na uwazi.
- Moyo wa Kujitolea (Volunteering Spirit): Wajumbe wa Baraza hujitoa kwa moyo wa kizalendo na si kwa maslahi binafsi, wakitoa muda na ujuzi wao kwa jamii.
- Usawa wa Kijinsia (Gender Balance): Baraza linatetea usawa wa jinsia kwa kutoa nafasi sawa kwa wanawake na wanaume katika uwakilishi na maamuzi.
- Uwezo wa Kubadilika (Adaptability): Baraza linaendelea kujiimarisha kwa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia, jamii na uchumi.
- Kushirikishana Maarifa (Knowledge Sharing): Baraza linahimiza upashanaji wa elimu na taarifa kwa kutumia lugha rahisi, zenye kueleweka kwa wananchi wote.

Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji Mkoa wa Morogoro, Bi. Potamia Buretta, alisisitiza kuwa nguzo hizo zimekuwa nyenzo muhimu ya kuwajengea wanakamati uwezo wa kuwawakilisha wananchi kwa ufanisi.

"Tunapotembelea wananchi, tunakuwa mabalozi wa maadili haya. Tunajua tunawakilisha umma, hivyo tunalazimika kuwa waadilifu, kusikiliza kwa heshima na kutoa mrejesho wa kweli. Hii ndiyo misingi ya utumishi wa umma," alisema Bi. Buretta.

Kwa kuzingatia misingi hii, EWURA CCC inaendelea kuwa chombo kinachoaminika na kinachojenga uwajibikaji wa watoa huduma katika sekta za nishati na maji, huku kikihakikisha sauti za watumiaji zinapewa kipaumbele.

# HabariPicha




*Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Kigamboni Bi. Francisca Kiwia, (wa kwanza kushoto), akielimisha walimu wa Shule ya Msingi Ungindoni juu ya matumizi sahihi ya umeme na maji.*



*Afisa Huduma kwa Wateja EWURA CCC Ruvuma Bi. Magreth Temba, Akielimisha kuhusu matumizi sahihi ya huduma za nishati na majii kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Lizaboni iliyopo Manispaa ya Songea.*



*Afisa Huduma kwa Wateja wa EWURA CCC Rukwa ndugu Ramadhani Kakende , akielimisha wananchi wa Mtaa wa Shule, Kata ya Chanji, Sumbawanga mjini, kuhusu kazi na majukumu ya Baraza.*



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji Mbeya, Bw. Lusekelo Joel Kajela, akielimisha wajasiriamali kutoka Kampuni ya Intel International (Tawi la Mbeya) kuhusu matumizi sahihi ya nishati safi ya kupikia, katika Ukumbi wa Tughimbe, Jijini Mbeya.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Kagera (wa pili kulia), Bw. Najim Bwanika akielimisha walimu na wanafunzi wa Shule Sekondari Rwamishenye, Manispaa ya Bukoba, kuhusu kazi na majukumu ya Baraza.*



*Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji, Kilimanjaro Bw. Muhsin Swai (aliyesimama), akielezea utaratibu wa kufuata wakati wa kuwasilisha malalamiko kwa EWURA katika kikao cha WDC kilichofanyika eneo la Samanga Hedikota, Kata ya Marangu Mashariki.*

ewura CCC
Consumer Consultative Council

# EWURA CCC ANTI-CORRUPTION POLICY

**1. Policy Purpose**

The purpose of this policy is to promote ethical conduct and prevent corruption within EWURA CCC. The policy establishes a framework for ensuring that all employees, Councilors, and stakeholders adhere to the highest standards of integrity and transparency in all operations and interactions.

**2. Scope**

This policy applies to all EWURA CCC Council members, employees, Regional Consumer Committee members, consultants, and any other individuals acting on behalf of the Council. It covers all aspects of EWURA CCC's operations, including financial management, procurement, decision-making, and interactions with external stakeholders.

**3. Definition of Corruption**

Corruption is defined as the abuse of power for personal gain, or the offering, giving, receiving, or soliciting of anything of value to influence the actions of an official in the discharge of their duties. This includes, but is not limited to:

- Bribery
- Deception
- Intimidation
- Conflict of interest
- Embezzlement
- Any other unethical or illegal activity that undermines transparency and accountability

**4. Commitment to Anti-Corruption**

EWURA CCC is committed to:

- Zero tolerance for corruption, bribery, or any form of unethical behaviour.
- Conducting its business in an open, fair, and accountable manner.
- Complying with all national and international anti-corruption laws and regulations.
- Promoting a culture of integrity, honesty, and ethical conduct within the Council.

**5. Responsibilities**

All EWURA CCC Councilors, employees, and RCCs are responsible for:

- Upholding the principles of this policy in all their actions.
- Reporting any suspected corrupt activities or unethical behaviour.
- Ensuring that their conduct is free from any conflict of interest or personal gain that compromises the integrity of EWURA CCC

.

**6. Reporting and Whistleblowing**

EWURA CCC encourages the reporting of any suspected corruption or unethical behaviour through established reporting channels, including:

- Anonymous reporting mechanisms (e.g., hotlines, and suggestion boxes installed at the regional offices)
- Reporting to supervisors.

The identity of whistleblowers will be protected, and EWURA CCC commits to taking appropriate action to investigate reports while ensuring confidentiality and protection against retaliation.

**7. Consequences of Violation**

Any Council Member, employee, RCC member, or stakeholder found to have engaged in corrupt activities will face disciplinary action, which may include termination, legal prosecution, and any other actions deemed necessary in accordance with national laws and EWURA CCC's internal regulations.

**8. Prevention and Awareness**

EWURA CCC will:

- Provide regular training and awareness programs on anti-corruption for Council Members and employees.
- Ensure that all stakeholders are aware of the policy and their responsibilities.
- Continuously monitor and assess risks related to corruption within the Council and take appropriate preventive measures.

**9. Policy Review**

This policy will be reviewed regularly and updated as necessary to ensure it remains effective and aligned with national and international anti-corruption standards.

**10. Effective Date**

The Policy was effected for implementation by the Council on 30th January 2025.



*Afisa Huduma kwa Wateja Mwandamizi wa EWURA CCC mkoa wa Mtwara, Ndugu Emmanuel Paul (kulia), akizungumza na mteja kuhusu haki na wajibu kwa watumiaji wa huduma za maji.*

# Sauti zilizopata haki: Wananchi wanavyonufaika na kazi za EWURA CCC

**Na Waandishi Wetu: Tanga, Rukwa na Mtwara**

Katika mazingira ambapo malalamiko ya watumiaji wa huduma za nishati na maji mara nyingi hayapati suluhisho la haraka, kuna sauti zinazothibitisha kuwa haki inawezekana pale ambapo kuna mwongozo sahihi. Sauti hizo ni za wananchi waliopata msaada kutoka Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC) na kuona maisha yao yakibadilika kwa hatua walizochukua.

Abdulsamad Shariff Attassy ni mmoja wa wananchi waliothibitisha kuwa haki huweza kupatikana. Mkazi huyu wa Barabara ya 18, jijini Tanga, alipata hasara kubwa baada ya umeme hafifu kusababisha uharibifu wa kifaa chake cha biashara jokofu yaani "Deep Freezer" ya kuhifadhi samaki.

"Ilikuwa ni hasara kubwa sana kwangu kama mfanyabiashara mdogo. Lakini nilipoelekezwa kufika EWURA CCC, ndipo nilipofungua ukurasa mpya wa matumaini," anasema Attassy na kuongeza kuwa, Baraza lilimsaidia kuwasilisha malalamiko rasmi kwa TANESCO kupitia EWURA, ambapo baada ya vikao vya usuluhishi, aliamriwa kulipwa Deep Freezer mpya. Leo, biashara yake inaendelea kama kawaida.

> **"Nilipojaribu kulalamika, nilikataliwa na TANESCO na kuambiwa kuwa ni lazima nilipe deni hilo. Lakini EWURA CCC walinipa usaidizi wa kitaalamu, wakaniwakilisha hadi suala hilo lilipopelekwa EWURA**

Naye Lucy Vundwe, mkazi wa Majengo, Sumbawanga, anakumbuka jinsi King'amuzi kilivyoungua kutokana na hitilafu ya umeme na kusema "Sikuwa najua pa kuanzia. Nilifikiria nitabeba tu mzigo huu. Lakini EWURA CCC walinielekeza kila hatua. TANESCO walinilipa fidia na sasa najua haki yangu," anasema Lucy na kuongeza kuwa, kwa msaada wa Baraza, Lucy alipata fidia kamili ya kifaa hicho, akithibitisha kuwa elimu na mwongozo vinaweza kuleta matokeo chanya.

Kwa upande wa Abubakari Mohamed kutoka Mtwara, anashuhudia changamoto tofauti. Anasema ndugu yake aliongezewa deni la kiasi cha shilingi 565,000 kwenye akaunti yake ya umeme, deni ambalo halikuhusiana naye, jambo lililomfanya aanze kukatwa pesa kila anaponunua umeme. "Nilipojaribu kulalamika, nilikataliwa na TANESCO na kuambiwa kuwa ni lazima nilipe deni hilo. Lakini EWURA CCC walinipa usaidizi wa kitaalamu, wakaniwakilisha hadi suala hilo lilipopelekwa EWURA," anashuhudia Abubakari. Baada ya uchunguzi, ilithibitika kuwa deni halikuwa halali. TANESCO walifuta deni hilo na kurejesha fedha zote zilizokuwa zimekatwa.

Kwa ujumla, ushuhuda wa wananchi hawa ni kielelezo hai cha kazi inayofanywa na EWURA CCC kuhakikisha sauti za watumiaji zinasikika na kulindwa.

Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji kutoka Mtwara, Bw. Said Twalibu, anasema "Kazi yetu si kusikiliza tu, bali ni kuhakikisha tunasimamia haki kwa vitendo. Ushuhuda kama huu unathibitisha kuwa uwepo wa Baraza una maana kubwa sana kwa wananchi."

Katika mazingira ambako changamoto za huduma bado zipo, EWURA CCC inaendelea kuimarisha jitihada zake za kuwahudumia wananchi kupitia elimu, msaada wa kisheria, na utetezi wa haki. Hii ni sauti ya mabadiliko. Hii ni nguvu ya ushirikiano. Na haya ni mafanikio ya watumiaji waliopaza sauti kwa ujasiri na kupata haki yao.

Maswali na Majibu

# Maswali yaulizwayo mara kwa mara

**Je, mteja alieyeuziwa mafuta machafu anatakiwa kulalamika EWURA ndani ya muda gani?**

Mteja ambaye ameuziwa mafuta yenye dosari anapaswa kuwasilisha lalamiko lake kwa EWURA ndani ya siku 7 tangu kutokea kwa tatizo.

Hii ni kwa mujibu Kanuni ya 26(1) ya Kanuni za EWURA za Kutatua Migogoro, 2020.

**Endapo mteja amesitishiwa huduma kwa kuchelewa kulipa bili anatakiwa kurejeshewa huduma ya maji ndani ya muda gani baada ya kulipa?**

Mtoa huduma atapaswa kurejesha huduma kwa mteja ndani ya saa 24 baada ya kulipa bili yote pamoja na gharama za kurejesha huduma. Endapo mtoa huduma atachelewa kurejesha huduma ndani ya muda huo, atawajibika kumlipa mteja fidia ya msingi kiasi cha shilingi 30,000/= na kiasi cha shilingi 5,000/= kwa kila siku itakayoongezeka baada ya masaa 24 kupita.

Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 34(3) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira (Ubora wa huduma na leseni), 2020.

**Je ni njia gani naweza kutumia kuwasilisha malalamiko EWURA?**

Zipo namna mbili unazoweza kutumia kuwasilisha malalamiko ambazo ni njia ya mtandao (electronic) na namna zinginezo, ikiwemo:-

- Kupiga simu ya EWURA: 0800 110 030 (bure)
- Kutuma barua pepe: info@ewura.go.tz
- Kujaza fomu ya malalamiko ya EWURA inayopatikana kwenye tovuti ya EWURA (www.ewura.go.tz)
- Kupitia kwa EWURA CCC

Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1-3) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro, (2020.

**Je naweza kusoma mita yangu ya maji kabla msoma mita hajaja?**

Ndiyo, unaweza kusoma mita yako ya maji kama ilivyoainishwa hapa chini lakini kwa aina zingine za mita usisite kuomba elimu ya usomaji mita kwa mamlaka husika ya maji.



# Maswali yaulizwayo mara kwa mara

**Mtu anayekusudia kufanya shughuli zinazodhibitiwa kama vile umeme, kisheria anatakiwa kuchukua hatua gani kabla ya kuanza shughuli hiyo?**

Anatakiwa kuwasilisha maombi ya leseni kwa mujibu wa utaratibu utakaowekwa na EWURA, na maombi hayo yaambatane na nyaraka zilizobatishwa katika Kanuni ya 5(1-3) ya Kanuni za Umeme (Shughuli za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji), 2024.

**Ni nini kifanyike endapo mtu atapata hasara ya maisha au mali kutokana na shughuli ya usambazaji wa gesi asilia?**

Mtu yeyote aliyepata hasara ya maisha au mali kutokana na shughuli ya usambazaji wa gesi ana haki ya kudai na kulipwa fidia na mmiliki wa leseni ya kuendesha huduma za gesi asilia.

Hata hivyo, mtu aliyepata hasara hiyo anatakiwa kwanza kuwasilisha malalamiko kwa mtoa huduma kwa lengo la kufikia suluhu kwa njia ya maelewano. Hiyo ni kwa mujibu wa Kanuni ya 26 (1-2) ya Kanuni za Mafuta (Gesi Asilia) (Huduma za Ugavi na Masoko) 2019.

**Je, sheria inasemaje kuhusu kuharibu miundombinu ya maji?**

Kifungu namba 61 cha Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019 kinaeleza ni kosa la jinai kuharibu miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira au mali za mamlaka ya maji, adhabu yake ni faini kuanzia Sh. 500,000/= hadi millioni 50 au kifungo cha miaka miwili hadi miaka mitano, au vyote kwa pamaoja.

**Je, ni adhabu ipi inaweza kutolewa kwa mtu akigundulika amechoma nguzo za umeme?**

Kifungu namba 61 cha Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019 kinaeleza ni kosa la jinai kuharibu miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira au mali za mamlaka ya maji, adhabu yake ni faini kuanzia Sh. 500,000/= hadi millioni 50 au kifungo cha miaka miwili hadi miaka mitano, au vyote kwa pamaoja.

Kanuni ya 6(1-3) ya Kanuni za Umeme (za Jumla), 2020, inataja adhabu inayotolewa kwa mtu aliyefanya uharibifu wa vifaa/miundombinu ya umeme ikiwemo nguzo, ni kuvirekebisha, kununua vingine vipya na kurejesha au kulipa fidia itakayokuwa imekokotolewa kulingana na uharibifu aliofanya.

**Kuna mkakati gani kuwawezesha watu kuelewa faida za kutumia nishati safi ya kupikia?**

Serikali imeandaa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034 kwa ajili ya kuwazesha watu kuelewa faida za kutumia nishati safi ya kupikia.

EWURA CCC ikiwa miongoni mwa wadau katika eneo hili imejipanga vyema kutoa elimu kwa umma kuhusu faida za kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuachana na matumizi ya nishati isiyo safi na salama.

Hii ni kwa mujibu, kifungu cha 4.1 cha Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034).

**Nani anawajibika kulinda umma dhidi ya hatari zinazoweza kusababishwa na shughuli za uzalishaji, usambazaji, na matumizi ya umeme?**

Kanuni ya 17(1) ya Kanuni za

ewura CCC
Consumer Consultative Council

# Maswali yaulizwayo mara kwa mara

Umeme za Jumla za mwaka 2020 inaipa TANESCO jukumu la kuhakikisha inazingatia usalama kwa umma dhidi ya hatari wakati wa kutekeleza shughuli zake za uzalishaji, usafirishaji, usambazaji, uuzaji wa umeme na ufungaji.

**Je mtu yeyote anaweza kuanza kujenga kiwanda cha kuchakata gesi asilia?**

Ndiyo, mtu yeyote anaweza kujenga kiwanda cha kuchakata gesi asilia kwa kuzingatia yafuatayo:-

a. Atawasilisha kwa EWURA michoro ya kina ya kiwanda hicho pamoja na vipimo vya sehemu zake;

b. EWURA imemjulisha mtu huyo kuwa ujenzi unaweza kuanza, kwa kuzingatia mabadiliko yoyote katika michoro au vipimo ambavyo EWURA itaona kuwa ni muhimu kwa sababu za usalama au za ulinzi wa mazingira; na

c. Mabadiliko yoyote yanayohitajika kwa mujibu wa aya (b) yamewasilishwa kwa EWURA.

Haya kwa mujibu wa Kanuni 19(1) ya Kanuni za Petroli (Uchakataji wa Gesi Asilia), 2019.

**Je, ni nani mwenye wajibu wa kudhibiti mivujo ya gesi asilia ikitokea?**

Kanuni ya 27(1) ya Kanuni za Petroli (Gesi Asilia Iliyoshindiliwa) (Huduma za Ugavi na Masoko), 2019 inampa jukumu la udhibiti mivujo ya bomba la gesi asilia mtoa huduma aliye na leseni ya EWURA

**Je, kuna sheria inayoipa mamlaka EWURA kufuatilia ubora wa huduma za maji?**

Ndiyo! Kifungu Na. 29(1)(e) cha Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019, inaipa nguvu EWURA kusimamia ubora wa huduma za maji yanayosambazwa na mamlaka za maji mijini.

**Kuna umuhimu gani wa kutumia Circuit breaker nyumbani?**

"Circuit breaker" ni kifaa kinachozima umeme haraka pale kunapotokea tatizo kama waya kugusana (short circuit) au kupita kwa umeme mwingi kupita kawaida. Inasaidia kuzuia ajali kama moto au kuharibu vifaa.

**Je ni muhimu kutumia mtaalamu wakati wa kutengeneza mifumo ya umeme (wiring) ndani ya nyumba?**

Ndiyo! Ni takwa la kisheria kwamba, mmiliki au mtumiaji wa jengo lazima amwajiri mtu mwenye leseni ya ufundi umeme kutoka EWURA kwa ajili ya kutekeleza kazi za ufungaji mifumo ya umeme. Hii ni kwa mujibuu wa Kanuni ya 19 (1) ya Kanuni za Umeme (Huduma za Ufungaji wa Umeme), 2022.

**Je, Kuna tofauti gani kati ya REA (Rural Energy Agency) na TANESCO (Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania)**

REA (Wakala wa Nishati Vijijini) ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Nishati Vijijini ya mwaka 2005. Kazi yake kubwa ni kuratibu na kufadhili miradi ya kupeleka umeme vijijini, kwa kushirikiana na TANESCO au wakandarasi wengine binafsi.

TANESCO (Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania) ni shirika la umma lililoanzishwa kwa jukumu la kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme kwa wateja wa Tanzania Bara.

Waweza kutembelea tovuti ya REA (https://rea.go.tz) pamoja na TANESCO (https://www.tanesco.co.tz) kujifunza zaidi.

# Maswali yaulizwayo mara kwa mara

**Je, kwa nini bei ya maji inatofautiana kati ya mamlaka moja na nyingine?**

Tofauti ya bei ya maji baina ya mamlaka moja na nyingine hutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo gharama halisi za uendeshaji za mamlaka husika, matengenezo, pamoja na uchakavu wa miundombinu ya maji katika mamlaka husika. EWURA husimamia na kupitisha viwango vya bei kwa kuzingatia utaratibu huo kama inavyoelezwa kwenye Kanuni ya 29, na sehemu ya nne yote (PART IV) ya Kanuni za EWURA za Maombi na Upangaji Bei, 2020.

**Mteja anaweza kufanya nini ikiwa TANESCO haina uwezo wa kugharamia ujenzi wa laini ya umeme endapo mteja anahitaji huduma hiyo?**

Endapo TANESCO haina uwezo wa kugharamia ujenzi huo, mteja anaweza kugharamia mwenyewe ujenzi wa laini yake ya umeme.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1-4) ya Kanuni za Umeme (za Jumla), 2020, Mteja atarejeshewa gharama hizo kupitia makato ya asilimia arobaini (40%) ya kila bili ya umeme au kila ununuzi wa umeme, kulingana na makubaliano na mtoa huduma. Marejesho hayo yataendelea hadi gharama zote zitakapolipwa kikamilifu. Hata hivyo, marejesho hayo hayatajumuisha gharama za laini ya huduma (service line) kama ilivyoidhinishwa na EWURA.

**Je, ninaweza kujiunganishia maji mwenyewe nikiwa na fundi na vifaa vyangu bila kusubiria watu wa mamlaka ya maji?**

Hapana! Kanuni ya 26(3) ya Kanuni za Usambazaji wa Maji, 2019 inatoa marufuku yakujiunganishia huduma ya maji pasipo kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka ya maji husika.

**Je EWURA CCC inaweza kuwasilisha lalamiko kwa niaba ya mtumiaji?**

Ndiyo, EWURA CCC ina uwezo wa kuwasilisha malalamiko kwa niaba ya mtumiaji au malalamiko yanayogusa watu wengi. Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 4(2&5) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro za mwaka, 2020.

**Je fomu maalumu za malalamiko zinapatikana wapi?**

Fomu maalumu za malalamiko zinapatikana kwenye ofisi za kanda za EWURA, ofisi za EWURA CCC na Kamati zake kote Tanzania Bara. Pia unaweza kupakua fomu hiyo kutoka kwenye tovuti ya EWURA www.ewura.go.tz au www.ewuraccc.go.tz

**Mteja wa umeme anakuwa na ushahidi gani kwamba amefungiwa umeme na fundi mwenye leseni ya EWURA?**

Kanuni Na.17(3) ya Kanuni za Umeme (Huduma za Ufungaji wa Umeme), 2022 inamtaka Fundi umeme kutoa Cheti baada ya kukamilisha zoezi la kufunga mfumo wa umeme nyumbani kwa mteja. Huu ndiiyo Ushahidi pekee anaokuwa nao Mteja.

**Je, mteja wa umeme anaweza kufunga mita za kupima matumizi ya umeme (submeter) kwa wapangaji?**

Ndiyo, mteja/mmiliki wa jengo anaweza kufunga mita ndogo ndogo (sub-meters) kwa madhumuni ya kubaini kiasi cha umeme kinachotumiwa na kila mpangaji.

Hii ni kwa mujibu wa Kanuni ya 14 ya Kanuni za Umeme (za Jumla), 2020

# Maswali yaulizwayo mara kwa mara

**Uniti moja ya maji sawa na lita ngapi za maji?**

Kwa kuzingatia vipimo vya ujazo, uniti moja ya maji ni sawa na lita elfu moja za maji. Hii ni sawa na ndoo hamsini za maji za lita ishirini.

**Je? kuna mwongozo wowote wa ukokotoaji wa bili za maji?**

Ndiyo, kuna mwongozo rasmi wa namna ya kukokotoa bili za maji, kama inavyoelezwa na Kanuni ya 2 ya Kanuni za EWURA za Uwasilishaji wa Maombi ya Bei na Uwekaji wa Viwango vya Bei za Huduma ya Maji, 2020.

Kanuni hizi zinaeleza kwa kina utaratibu wa watoa huduma za maji kuwasilisha maombi ya bei kwa EWURA, namna ya kuidhinisha viwango hivyo, na misingi inayotumika kukokotoa gharama halali ambazo mtumiaji anatakiwa kulipa.

Vigezo vinavyotumika ni pamoja na kiasi cha maji kilichotumika (kupitia mita), gharama za uendeshaji, matengenezo, na uwekezaji unaohitajika ili kuboresha huduma.

Kwa hiyo, bili ya maji haikokotolewi kiholela, bali inafuata taratibu zilizowekwa kisheria ili kuhakikisha mtumiaji analipa kwa haki kulingana na matumizi halisi na gharama halali za utoaji huduma.

**Je, ni hatua gani za kufuata ikiwa mteja anataka kuhamisha mita yake ya maji kutoka ndani ya nyumba na kupeleka nje, na kuna gharama zozote mteja atapaswa kulipia?**

Hatua za Kufuatwa ili kuhamisha laini ya huduma (service line) kwa mteja aliyeomba  utafanywa na mamlaka ya maji kwa gharama za mteja, ambapo mteja atahitajika kuwasilisha maombi kwa mamlaka ya majikwa kujaza fomu maalum au kuwasiliana na ofisi za huduma kwa wateja na Mamlaka ya maji itafanya uhakiki wa eneo la sasa na eneo jipya ambalo mita itahamishwa. Hii inajumuisha tathmini ya uwezo wa eneo jipya kwa ajili ya kuweka mita na vilevile hali ya miundombinu ya maji.

Mteja atalazimika kulipia gharama za uhamishaji, ambazo zinaweza kujumuisha malipo ya kazi ya ufundi, vifaa, na ufungaji. Gharama hizi zinaweza kutofautiana kulingana na umbali wa uhamishaji, aina ya mita, na hali ya miundombinu. Kanuni ya 39(1) (a) ya Kanuni za Ubora wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira (Ubora wa huduma na leseni), 2020

**Je, ni kwa nini umeme hukatika mara kwa mara katika baadhi ya maeneo?**

Kwa mujibu wa Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa TANESCO, Umeme unaweza kukatika mara kwa mara kutokana na Katizo lililopangwa linalofanywa na TANESCO kwa ajili ya kufanya matengenezo ya miundombinu, maboresho ya mitambo, au uunganishaji wa laini mpya. Kwa katizo la namna hii TANESCO huwajibika kuwajulisha wateja siku kumi kabla. Katika taarifa ya katizo hili, taarifa huonesha muda wa katizo kutokea, maeneo yatakayoathirika, sababu ya katizo na muda utakao chukua kwa huduma kurejea.

Katizo lisilopangwa hutokea ghafla bila taarifa kutokana na hitilafu za kiufundi, kuharibika kwa vifaa, mvua kubwa au upepo mkali, ajali za magari kugonga nguzo, wizi wa nyaya, au mzigo mkubwa kupita uwezo wa mtambo. Katizo hili huwa changamoto zaidi kwani linaweza kuchukua muda mrefu kurekebishwa kulingana na ukubwa wa tatizo.TANESCO huwajulisha wateja wake sababu ya katizo ndani ya masaa 24.

# Maswali yaulizwayo mara kwa mara

**Ni nani mwenye wajibu wa kuhakikisha mita ya umeme imehakikiwa na Wakala wa Vipimo kabla ya kutumika kwa mteja?**

Mtoa huduma ya umeme, yaani TANESCO ndiye mwenye wajibu wa kuhakikisha mita ya kupimia matumizi ya umeme ya mteja imehakikiwa na Wakala wa Vipimo. Hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 46 ya Kanuni za Umeme (Huduma za Ugavi), 2019.

**Nishati safi ya kupikia ni nini? Kwa nini serikali inasisitiza kutumia nishati safi ya kupikia?**

Nishati safi ya kupikia ni aina ya nishati inayotumiwa kwa kupikia chakula ambayo haina madhara kwa afya ya binadamu wala mazingira. Nishati hii hutoa moshi kidogo au hakuna kabisa, ina uwezo mkubwa wa kupikia haraka, na ni salama kwa watumiaji. Hii inajumuisha gesi asilia, gesi itokanayo na petroli yaani LPG, umeme, bayogesi, mkaa mbadala, bayoethano, majiko banifu na majiko ya nishati ya jua.

Kutumia nishati safi hupunguza hatari za kiafya kama magonjwa ya njia ya upumuaji, inalinda mazingira kwa kupunguza ukataji miti, na huokoa muda na gharama kwa watumiaji.

**Je, EWURA inatumia vigezo gani kupanga bei za umeme?**

Baada ya kupokea maombi ya kubadilisha bei za umeme kutoka kwa mtoa huduma, EWURA hutumia vigezo mbalimbali katika kupanga bei za umeme, zikiwemo gharama halisi za uzalishaji, usafirishaji, usambazaji, na maslahi ya watumiaji. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 17(1-2) cha Sheria ya EWURA, Sura Na. 414.

**Ni kwa namna gani wananchi wanashirikishwa kutoa maoni kuhusu mabadiliko ya huduma zinazodhibitiwa na EWURA?**

Wananchi wanashirikishwa kutoa maoni kuhusu huduma zinazodhibitiwa na EWURA kupitia kifungu namba 19 (2&4) cha Sheria ya EWURA sura 414. Hii husaidia kuongeza uwazi na kuhakikisha maamuzi yanazingatia sauti za wadau mbalimbali, wakiwemo watumiaji wa huduma husika.



Maswali na Majibu

ewura CCC
Consumer Consultative Council

# Nukuu Maridhawa

"Masuala ya maji sasa yamekuwa ajenda muhimu za kisiasa duniani kote. Ni lazima tuanze kuyashughulikia sasa ili tuwe tayari kwa kesho

*-- Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

"Ni jukumu la mamlaka husika kufanyia kazi changamoto hii ili kuhakikisha maji yanayozalishwa yanawafikia watumiaji kuzipunguzia mamlaka gharama za uendeshaji.

*-- Mhe. Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati*